

MADA:

// UHAKIKI WA FANI KATIKA TAMTHILIA ZA K.W.

WAMITILA.

NA:

| MWANGI DUNCAN KAHIRO

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI
YA MAHITAJI YA SHAHANDA YA UZAMILI (MASTER
OF ARTS) KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

2005.

JOMO KENYATTA MEMORIAL
LIBRARY

University of NAIROBI Library



0496772 5

UNGAMO


TASNIFU HII NI KAZI YANGU BINAFSI NA
HAIJATOLEWA KWA MAHITAJI YA SHAHADA
KATIKA CHUO KIKUU KINGINE CHOCHOTE.

Mwangi

KAHIRO MWANGI DUNCAN

(MTAHINIWA)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yangu
nikiwa msimamizi wa kazi hii niliyeteuliwa na chuo
kikuu

A handwritten signature in black ink, appearing to read "Ndgi. Gichobi B. Mungania", is written over a horizontal line. The signature is fluid and cursive.

Ndg. Gichobi B. Mungania

TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia mpenzi mke wangu, Esther Njambi pamoja na watoto wangu.,
Herbert Kahiro, Stella Murugi na Angela Wanjiru (Ciru).

SHUKRANI

Ni watu wengi ambao walichangia katika kuhitimu kwangu, hasa katika kuhitimisha tasnifu hii. Kwanza ningependa kumshukuru msimamizi wangu, - Basilio G. Mungania kwa msaada wake mwingu na wa kitaaluma ambao ulinifaidi sana wakati wa kuiandika tasnifu hii.

Ningependa pia kuwashukuru wahadhiri wa idara ya Isimu na lugh za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Nairobi. Hawa ni Dkt. Mbatia, Ndg. Arege, marehemu Ndg. Mugullu, Prof. Abdulaziz na Dkt. Orali. Hawa walichangia kwa njia moja au nyingine kwani ushauri wao wakati wa mihadhara uliniwezesha kuipata mada ya kuandikia na pia uelewa ufaao.

Nisingependa kuwasahau tuliongo'a nanga nao kuogelea katika bahari ya elimu ambayo wengi wanaiogopa. Hawa ambao tulitiana shime na kuhimizana wakati wa machafuko baharini ni: Mutua Ndolo, Evans Bogoruko, Sara Manzi, Otieno, Grace Gathoni, Jane Ochoki na Eunice Nangila. Wote hawa nawashukuru kwa mchango wao wakati wa mihadhara.

Sitamsahau pia Mungai na Nyambunga ambao walikuwa mwaka mmoja nyuma yangu. Hawa walinisaidia sana kwa kunipa vitabu vyao vyta kusoma wakati wa kuandika tasnifu yangu.

Shukrani za kipekee ni kwa bibi mpenzi, Njambi, ambaye alinipa moyo na kuniliwaza wakati wote na hasa katika kipindi cha kozi hii. Alinipa motisha iliyonifanya kujitahidi na alihakikisha kuwa nina amani ifaayo wakati wote wa masomo yangu.

Kwa wote niliowataja, ninarudia tena shukrani na Jalali awanemeeshe ili muweze kuwasaidia na kuwafaa wengine maishani.

IKISIRI

Tasnifu hii ni uhakiki wa fani katika tamthilia za Kiswahili ambazo zimetungwa na Wamitila, K.W. Tamthilia hizi ni *Wingu La Kupita* (1999) na *Pango* (2003). Katika tahakiki yetu, tumeteua na kujadili vipengele maalum vya fani. Kazi ina sura tano.

Katika sura ya kwanza, tumeelezea dhana za kimsingi zinazohusiana au kupatikana katika somo hili. Dhana hizi ni pamoja na: fani na tamthilia. Tumeelezea pia msingi wa kinadharia tulioatumia, sababu za kuchagua mada hii na upeo na mipaka yake. Tumeweza kurejelea kazi za fasihi zilizowahi kuandikwa zikiangazia fani.

Sura ya pili ni kuhusu ujumla na mjengo wa ploti. Katika sura hii tunaeleza dhana ya ploti. Vipengele ambavyo tumejadili ni mfululizo wa vitushi na jinsi vinashirikiana katika kuleta umoja wa kazi na tumetoa tathmini yetu kuhusu ploti katika kila tamthilia.

Katika sura ya tatu tumeshughulikia umbuji wa wahusika. Tumejadili jinsi wahusika mbalimbali walivyochorwa katika tamthilia, nafasi au majukumu yao na mchango wanaotoa katika uendelezaji wa kazi.

Katika sura ya nne, tumehakiki matumizi ya lugha katika kazi za Wamitila. Tumeangalia jinsi lugha imetumiwa katika mazingira mbalimbali na inavyotumiwa na wahusika wa umri mbalimbali. Tumejadili pia usanaa na ujumi wa lugha iliyotumiwa.

Sura ya tano ni ya hitimisho na mapendekezo. Katika sehemu hii tumeangaza kimukhtasari zile sifa baininifu zinazojidhihirisha katika ujumla wa fani katika kazi za Wamitila kama tulivyoweza kuzijadili na kuzihukumu. Uhakiki wetu umechambua udhaifu au ufanifu wa mtunzi katika umbuji wa wahusika na lugha. Tumeweza kutoa mapendekezo katika tasnifu kuhusu kazi tulioifanya.

YALIYOMO**UKURASA**

UNGAMANO -----	I
TABARUKU -----	II
SHUKRANI -----	III
IKISIRI -----	IV
YALIYOMO -----	V
SURA YA KWANZA -----	1
1.0 Utangulizi -----	1
1.01 Somo La Utafiti -----	2
1.02 Madhumuni Ya Tasnifu -----	3
1.03 Sababu Za Kuchagua Somo -----	3
1.04 Mipaka Na Upeo Wa Somo -----	4
1.05 Nadharia Tete -----	4
1.06 Yaliyoandikwa Kuhusu Somo -----	4
1.07 Msingi Wa Kinadharia -----	6
1.08 Njia Za Utafiti -----	9
SURA YA PILI -----	10
2.00 Ploti -----	10
2.01 Utangulizi -----	10
2.02 Ploti Katika Wingu La Kupita -----	13
2.03 Tathmini -----	18
2.04 Ploti Katika Pango-----	23
2.05 Tathmini -----	28

2.06 Hitimisho -----	32
SURA YA TATU	
3.00 Umbuji Wa Wahusika -----	32
3.01 Utangulizi -----	32
3.02 Wahusika Katika <i>Wingu La Kupita</i> -----	33
3.03 Wahusika Wakuu -----	34
3.04 Wahusika Wadogo -----	38
3.05 Tathmini -----	42
3.06 Wahusika Katika <i>Pango</i> -----	42
3.07 Wahusika Wakuu -----	43
3.08 Wahusika Wasaidizi -----	46
3.09 Tathmini -----	49
 SURA YA NNE -----	51
4.00 Matumizi Ya Lughya -----	51
4.01 Utangulizi -----	51
4.02 Lughya Katika <i>Wingu La Kupita</i> -----	53
4.03 Lughya Ya Vijana -----	54
4.05 Lughya Ya Wazee Wa Makamo -----	58
4.06 Matumizi Ya Lughya Kitamathali Katika <i>Wingu La Kupita</i> -----	62
4.07 Matumizi Ya Lughya Katika <i>Pango</i> -----	71
4.08 Lughya Ya Vijana -----	71
4.09 Lughya Ya Wazee -----	74
4.10 Lughya Katika Mazingira Na Muktadha Maalum Katika <i>Pango</i> -----	77
4.11 Matumizi Ya Lughya Kitamathali -----	79

SURA YA TANO

5.00 Hitimisho Na Mapendekezo -----	82
5.01 Hitimisho -----	82
5.02 Mapendekezo -----	85
Marejeleo -----	86

SURA YA KWANZA

1.00 UTANGULIZI

Tamthilia ni mojawapo ya tanzu kuu za fasihi andishi. Zile zingine ni riwaya na ushairi. Dhana ya tamthilia ina msingi wake katika kitenzi “mithilisha” yaani kuiga.

Tamthilia kwa hivyo ni utanzu wa kifasihi unaohusika na uigizaji. Tamthilia huwa na sifa kuu za kimuundo na kimtindo zinazoitofautisha na kazi za tanzu zile zingine kama vile riwaya na ushairi. Kwanza mpangilio wa sehemu pamoja na vitushi vinavyojenga kisa cha tamthilia. Tamthilia imegawanywa katika sehemu, maonyesho na matendo.

Tamthilia inahusu makundi matatu ili iweze kukamilika. Makundi hayo ni mtunzi, waigizaji na hadhira. Hivyo, ingawa mpangilio wa tamthilia huiwezesha kusomeka kama kazi zingine za fasihi zilizo katika maandishi, malengo asilia ya mtunzi wa kazi ya tamthilia ni kubuni kazi ya kisanaa inayoweza kuigizwa katika jukwaa na wahusika halisi ili itazamwe na hadhira halisi. Kwa hivyo, tamthilia inaweza kuelezwa kama sanaa tendaji.

Kazi tunazozishughulikia katika utafiti wetu zimo katika kundi hili la utanzu wa tamthilia. Kwa vile uhakiki wetu unajikita kwenye fani, itakuwa vyema kueleza dhana hizi mbili yaani: uhakiki na fani.

Mbatia, M. (2000:89) katika *Kamusi Ya Fasihi* amefasili uhakiki hivi:

Jumla ya hatua za kuichunguza kazi ya fasihi kitaalamu.

Hatua hizo zinahusu uchamumbuzi, ufasiri, ufanuzi, utathmini, ulinganishi na utoaji hukumu juu ya kufeli au kufaulu kwa mtunzi wa kazi husika katika jaribio lake la kubuni sanaa.

Mtaalamu mwingine Mbunda Msokile (99:VI) kwa kuzingatia jukumu la mhakiki anasema kwamba:

Mhakiki humtahadharisha msanii kuhusu makosa
aliyofanya katika kuikabili kazi yake na hivyo
kumwezesha awe na nafasi nzuri zaidi ya kuirekebisha
au kuwa na makini zaidi wakati wa kuishughulikia
kazi nyingine

Kwa hivyo uhakiki wapaswa uwe wa kitaalamu na mwishowe mhakiki atoe tathmini yake juu ya kazi anazozishughulikia kwa kuzingatia kaida za utunzi katika utanzu unaohusika.

Kipengele tunachoingatia katika uhakiki wetu ni kile cha fani. Ingawa tunakiita kipengele, kina vipengele kadhaa ndani yake. Kama anavyosema Senkoro (1983: 28)

Fani ni vipengele vya kazi ya kisanaa
Vinavyojenga umbo la kazi ya kisanaa.

Mbatia, M (2001: 13) anasema:

Fani ni jumla ya vipengele vya kimtindo
na kisanaa katika kazi ya kifasihi vinavyojenga
kiunzi cha kubebbea ujumbe na maana mahsus

Wataalamu wengine wametoa fasili zao lakini kuna maafikiano ya fasili zao kwamba, fani ni vile
vipengele vya kisanaa ambavyo kwa pamoja hujenga umbo la kazi ya kisanaa. Hivyo fani huwa ni
mjumuiko wa vipengele mbalimbali vya kisanaa ambavyo huchangia katika ukamilifu wa kazi
maalum. Kufeli au kufaulu kwa mtunzi hutegemea jinsi alivyovipanga vipengele vyake katika
kupitisha ujumbe wake. Kila mtunzi ana jinsi yake ya kuvipanga vipengele hivyo na tofauti hizi za
jinsi watunzi wamevipanga vipengele hivyo ndiko kunakosababisha kila mmoja kuwa na fani
tofauti na ya mwininge.

1.01

SOMO LA UTAFITI

Uchunguzi wetu ni tahakiki ya fani katika tamthilia mbili zilizotungwa na Wamitila. Tamthilia hizi
ni:- *Wingu La Kupita* (1999) Na *Pango* (2003). Katika utangulizi tumebainisha kuwa, lengo la
mtunzi ni kupitisha ujumbe fulani kwa hadhira yake. Tumeeleza kuwa, kila mtunzi ana njia yake
maalum ya kupitisha ujumbe huo katika uandishi wake kulingana na lengo alilonalo. Katika
uchunguzi wetu tumechunguza jinsi alivyoteua na kutumia vipengele mbalimbali vya fani, uhusiano
wa kisanaa wa vipengele hivyo, athari, pamoja na mchangano wake. Tutatoa tathmini yetu kuhusu
ufanifu au udhaifu wa kifani kama unavyojitokeza katika kazi yake.

Ingawa kazi ya fasihi huwa na vipengele aina aina vinavyoweza kufanyiwa uhakiki, tumechagua fani
kwa vile ndio hutawala uwasilishaji, ushikamano na uhusiano wa kuwathiriana kwa vipengele
mbalimbali vya kisa katika kazi ya fasihi.

Kwa kuwa fani ni ujumla wa matumizi ya lugha, usawili wa wahusika, wa kisa, mpangilio wa
vitushi, pamoja na uchoraji wa mandhari na ploti. Fani ndiyo husaidia kufanikisha maudhui ya

mtunzi. Kuitalii fani kwa hivyo ni kama kuchanganua zile sehemu kuu zinazojenga kazi ya fasihi.

Kila mtunzi huwa na njia yake ya kujumuisha vipengele vya fani ili kuwasilisha ujumbe wake.

Mtunzi anaweza kuunganisha vipengele vya fani vizuri au vibaya, na hivyo kazi yake ikawa yenye fani pevu au fani finyu. Na hivyo kuifanya kazi yake iwe ya kuvutia kwa msomaji wake au ya kuchosha msomaji. Hivyo, inafaa mtunzi ajumuishhe vipengele mbalimbali vya fani vizuri ili aweze kuwa na ukamilifu ufaao wa kazi yake. Kwa hivyo katika uchunguzi wetu wa tamthilia za Wamitila, *Wingu La Kupita* na *Pango*, tumechunguza jinsi ameunganisha vipengele vya fani katika kupertisha ujumbe wake.

1.02

MADHUMUNI YA TASNIFU

Madhumuni ya tahakiki yetu ni kutathimini vipengele tofauti vya fani katika tamthilia za K.W.

Wamitila *Wingu La Kupita* na *Pango*. Azma yetu ni kuweza kubainisha ufanifu ama udhaifu ulioko wa umbuji wa vipengele vya fani katika kazi hizi kwa kuzingatia kaida za utanzu wa tamthilia.

Tutachukulia ufanisi wa fani kama dhihirisho la umahiri na ukomavu wa mtunzi katika kuteua na kutumia vipengele vya fani kwa kuzingatia kaida za utanzu huu na udhaifu kuwa ile hali ya kutozimudu na kutowitawala vile vipengele vya fani kwa kuzingatia kaida za utanzu huu na pia kama ile hali ya kutozimudu na kutowitawala vile vipengele vya fani ambavyo vilikusudiwa kujenga kazi za kisanii.

1.03

SABABU ZA KUCHAGUA SOMO

Sababu ambazo zilitupelekea kuzifanya uhakiki kazi hizi za Wamitila ni: kwanza kazi hizi mbili hazijafanyiwa uhakiki wowote kwa hivyo tunataka kuliziba pengo hili.

Pili: Mtunzi ni mwandishi mpya katika utanzu wa tamthilia na anaweza kuwa ameibuka na mitindo mipyia ya utunzi katika tamthilia za Kiswahili.

Tahakiki yetu inahu tamthilia mbili za Wamitila yaani *Wingu la kupita na Pango*.

Tumeshughulikia vipengele vitatu vya fani katika kila moja ya kazi hizi. Tumejadili uumbaji wa ploti, wahusika na matumizi ya lugha. Katika usawiri wa wahusika tumeangalia sura wahusika wanamojitokeza na uhalisia wao, nafasi wanazochukua na michango yao katika kujenga umbo la kazi nzima. Tumeangalia jinsi lugha imetumiwa na wahusika mbalimbali na jinsi inavyooana na mazingira mbalimbali.

Tumezingatia pia kipengele cha ploti kama kinavyodhihirika katika kazi hizi. Hapa tumeangalia jinsi mfululizo wa visa pamoja na mpangilio wa sehemu ambazo zinajenga visa mbalimbali.

1.05

NADHARIA TETE

Uhakiki wetu umeongozwa na nadharia tete hizi:

- (i) Uteuzi pamoja na matumizi ya fani ya mwandishi imechangia katika ama ufanifu au udhaifu wa kazi zake.
- (ii) Tamthilia ya pili yaani *Pango* ina fani pevu kushinda ya kwanza.
- (iii) Mtunzi amefuata kaida za utunzi wa tamthilia kama vile tararuki, uhalisia wa ploti, mshangao na kadhalika vyema katika kazi yake.

1.06

YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO

Uwanja wa fani umeandikiwa na wataalamu na wahakiki mbalimbali.

Mbatia (2001: 1) Katika *Kamusi Ya Fasihî* ametoa fasili ya fani kama jumla ya vipengele vya kimtindo na kisanaa katika kazi ya kifasihi vinavyojenga kiunzi cha kubebea ujumbe na maana mahsus. Mbatia ametoa fasili tu ya fani katika kamusi yake lakini sisi tutakuwa tukichunguza jinsi vipengele hivyo vya fani yaani ploti, wahusika na matumizi ya lugha alivyovitaja viliviyotumiwa na Wamitila katika tamthilia zake mbili ili kufanikisha ujumbe wake. Ndung'u (1996) ameshughulikia fani katitika riwaya za Katama Mkangi.

Kwa upande wetu tumeshughulikia fani katika tamthilia na sio katika riwaya ingawa kazi ya

Ndung'u itatufaa katika utafiti wetu kwa vile anajishughusha na fani.

Kiteki (1998) amehakiki fani katika tamthilia za Emmanuel Mbogo. Kiteki ameshughulikia vipengele vya ploti na uunbaji wa wahusika. Vipengele hivi vina umuhimu katika kazi yetu kwa vile hata sisi tunashughulikia vipengele hivyo ingawa katika tamthilia tofauti. Naye Mwangangi Musyoka (1996) amehakiki fani katika tamthilia za Jay Kitsao katika tasnifu yake. Ameshughulikia vipengele vya uumbaji wa wahusika, ploti na matumizi ya lugha katika tamthilia hizo. Tahakiki hii yake itakufaa kwa vile hata sisi tunavishughulikia vipengele hivyo vya fani katika tamthilia za Wamitila.

Msokile (1993:33) katika *Misingi Ya Uhakiki Wa Fasihi* ameshughulikia muundo wa kazi za fasihi ambapo ametoa ufanuzi wa muundo na kutaja aina nne za muundo. Ingawa hivyo, maelezo yake ni ya jumla tu lakini sisi tumejihuisha na muundo katika kazi mahsus na hivyo tumezama zaidi kuliko alivyofanya yeye Msokile. Katika kitabu hicho, (uk. 32-35) Msokile ameshughulikia kipengele cha wahusika kwa kutoa maelezo ya jumla tu na kutaja aina mbalimbali za wahusika. Ingawa amekishughulikia kipengele hicho ambacho hata sisi tumekishughulikia, sisi tumejikita katika kazi za mwandishi fulani na hivyo lazima tuzame zaidi katika kipengele hiki kuliko alivyofanya yeye Msokile.

Senkoro (1987:85-90) katika *Fasihi Na Jamii* ameshughulikia fani lakini kwa kutoa mawazo ya wataalamu mbalimbali na hivyo akawa hajihuishi na vipengele vyovyote maalum vya fani. Sisi tunashughulikia fani katika kazi mahsus kwa kuzingatia vipengele vya fani na jinsi vinavyotumika katika kuwasilisha ujumbe katika kila moja ya kazi hizo. Mazrui na Syambo (1992) katika *Uchambuzi Wa Fasihi* wameeleza nguzo za tamthilia kwa kutaja ploti, aina za wahusika na lugha. Wao wamevieleza vipengele hivi kwa kuvitenganisha. Ingawa hivyo maelezo hayo yatatuzaa katika kazi yetu . lakini sisi tutaangalia jinsi wahusika wanavyoitumia lugha na kusukuma ploti mbele.

Katika tasnifu yetu tunahakiki fani katika tamthilia za Wamitila na tumeteua vipengele vya uhusika, ploti na matumizi ya lugha. Tutaangalia muumano, uhusiano na utangamano wa vipengele hivyo vya fani katika ujenzi wa kazi hizi mbili. Tumeshikilia kwamba, fani ni upekee wa mtindo kama asemavyo Senkoro (1987) katika *Fasihi* kuwa: mtindo ni upangaji wa fani na maudhui katika kazi ya fasihi kwa njia ambayo mwishowe hujitokeza au huonyesha unafsi na upekee wa mtungaji wa kazi hiyo. Kama ambavyo amesema, sisi pia tunataka kutathmini ufanisi au udhaifu wa fani katika tamthilia mbili za Wamitila.

1.07

MSINGI WA KINADHARIA

Uhakiki wetu utaongozwa na nadharia ya umuundo. Umuundo unahuishwa na wanaisimu wa shule ya Prague. Hivyo ina misingi yake katika Isimu na ilianza kutumika katika uhakiki wa kifasihi kwanza mwaka wa 1920. Wanamuundo walichunguza muundo wa ndani wa kazi za kifasihi hasa za kishairi ambazo walishughulikia zaidi kuliko kazi zingine.

Hivyo, waanzilishi wa nadharia hii walishughulikia ushairi zaidi kuliko kazi zingine. Wao walidhamiria uhakiki uweze kutilia fani maana zaidi kuliko maudhui yaliyo katika kazi ya kifasihi. Wahakiki wanaofuata nadharia hii ya umuundo hushikilia ufanifu wa kazi ya kisanaa hutokana na mtazamo kwamba ingawa kazi ya fasihi inaweza kukosa maudhui muhimu, utaaluma wa kisanii katika kazi hiyo unaweza kudhahirika katika fani iliyotumiwa na mtunzi.

Wanamuundo hushikilia kuwa, lazima mhakiki ajifunge kwenye kazi ya kifasihi bila kujihusisha na kitu kingine nje ya kazi hiyo. Culler (1975: 46) anaunga mkono mtazamo huu kwa kuelaza kuwa uhakiki uweze kubainisha mifumo ya kindani ya sanaa inayoviwezesha viungo vyake vya fani kuwa na taathira katika kazi ya fasihi. Hivyo, fasihi hupaswa kuhakikiwa kama sayansi inayojisimamia kwa kuvirejelea viungo vyake vya pekee bila kuyahusisha maswala yaliyo nje.

Wamitila (2002: 17) anaunga mkono hoja hii ya fasihi kuhahakikiwa kama sayansi anoposema:

Wana –umuundo waliamini kuwa mhakiki hawezikufanikiwa kwenye kazi yake bila ya kutumia mkabala wa kimethodolojia.

Mwelekeo wa uhakiki wa kimuundo ni kufafanua kazi za kifasihi bali sio kuzifasili. Kimsingi, uhakiki huu unajihuisha na kuchunguza vipengele mbalimbali vya fani na kuonyesha jinsi vinavyounda umbo la kazi nzima. Umuundo unawekewa msingi na mawazo ya mwana-isimu Ferdinand de Saussure. Kwa hivyo nadharia yenewe ina misingi yake katika isimu na inatumia taratibu za kiisimu kama vile 'Langage', 'Langue' na 'Parole'.

Nadharia hii ina husiana na isimu kwa kiasi kikubwa. Mawazo ya Mwanaisimu Ferdinand de Saussure yana athari kubwa katika ukuaji wa nadharia hii. Katika nadharia hii lugha hutazamiwa kama mfumo au muundo ulio na vipengele mbalimbali ndani yake. Hivyo hivyo fani ambayo ni muundo wa kazi fulani ya kifasihi ina vipengele mbalimbali kama vile. ploti, wahusika, matumizi ya lugha na kadhalika. Mwana – isimu huyu Ferdinand de Saussure alitumia dhana mbili muhimu katika kazi yake na ni dhana ambazo ziliwasaidia wana-umuundo katika kuelewa miundo ya kazi za kifasihi

Istilahi alizobuni mwana-isimu huyu ni ‘Langage’, ‘Langue’ na ‘parole’: Ferdinand alieleza ‘Langage’ kama kipawa cha usemi ambacho kila binadamu asiye na upungufu wa kusema huwa nacho. Kipawa hiki kinatokana na urithi wa kuzawa. Dhana hii inasimamia lugha zote kwa jumla. Kwa hivyo tunaweza kuichukulia ‘Langage’ kama fasihi zote za kilimwengu. ‘Langue’ ni mfumo dhahania wa lugha fulani ambao hutumiwa na jamii fulani. Mfumo huu wa lugha hujengwa na vipashio mbalimbali ambavyo huhusiana. Kwa hivyo ‘langue’ ama mfumo – lugha ni mfumo changamano ambao ndani yake kuna mifumo kadhaa kama vile: fonolojia, sintaksia, semantiki na mofolojia. Mifumo hii huhusiana na hukamilishana sawa na ambavyo vipengele vya fani huwa.

Kulingana na Ferdinand de Saussure basi tunapochunguza muundo tunachunguza jinsi vipengele vidogo vya kitu vinavyo shirikiana kukiunda kitu kizima. “Langue” huchukuliwa kuwa kama mfumo wa fasihi fulani kama vile ya Kiswahili. Kama vile mfumo lugha (langue) ulivyo na kanuni na kaida zake, hivyo ndivyo fasihi fulani inavyojisimamia kama ilivyo ‘langue’! Kama ambavyo vipengele

mbalimbali nya mfumo lugha hushirikiana kuunda mfumo-lugha (langue) kuna vipengele mbalimbali nya matini ambavyo mtunzi huvileta pamoja katika utunzi wake ili jkujenga kazi mahsusni.

Hivyo katika kuhakiki kazi ya mtunzi kifani, tunaangalia vipengele nya fani alivyotumia na jinsi vinavyoshirikiana katika kubuni umbo la kazi nzima. Dhana ya “parole” inarejelea ule usemajni wenyewe wa lugha ambaa hufanywa na kila mtu. Hili ni tendo la mtu binafsi, yaani ule upekee wa msemaji katika kuitumia lugha. Wasemaji wa lugha, kama vile ya Kiswahili, huwa na umahiri tofauti katika usemajni wao. Katika fasihi, ‘parole’ ni sawa na tungo za wasanii mahsusni. Tungo zao zinawakilisha sifa na kanuni za utunzu unaohusika. Kama “parole” ilivyo matumizi ya lugha ya mtu binafsi, ndivyo kila mtunzi alivyo na umbuji wa kipekee ulio tofauti na wa mwingine. Umbuji wake waweza kuwa wa kufanikisha au kushusha fani katika kazi yake au kazi zake.

Kwa hivyo tumetumia vipengele nya ‘langue’ na ‘parole’ nya nadharia ya umuundo katika uhakiki wetu. 'Langue' tumeichukulia kuwa mfumo mzima wa fasihi fulani kwa mfano ya Kiswahili na 'Parole' kama kazi mahsusni ya mtunzi fulani.

Katika kuzihakiki tamthilia hizi mbili za Wamitila kifani, tumetumia njia mbalimbali. Kwanza tumezisoma kazi ili tuweze kupata nguzo za kufikia uhakiki mpevu na wenyewe ithibati za kisanaa. Tumefanya utafiti katika maktaba kwa kutalii na kurejelea maoni ya wengine, hasa wataalamu waliochangia katika utanzu wa drama ili tuweze kumtafutia nafasi anayostahili katika uwanja wa sanaa hasa utanzu wa tamthilia.

SURA YA PILI

2.00 PLOTI

2.01 UTANGULIZI

Wataalamu mbalimbali wametoa fafanuzi zao juu ya ploti. Fafanuzi hizo zinalenga katika maana, umuhimu na matazamio yaliyopo kuihusu ploti inayofaa katika utunzi wa kisanaa.

Syambo na Mazrui (1992:77) wameifasili ploti kama:

Mfuatano wa matukio yanayojenga kazi ya kifasihi na sababu zake.

Katika kuoyesha umuhimu wa ploti katika kazi za kisanaa, wameifananisha na ramani katika safari. Kwa hivyo, umuhimu wa ploti ni kumwongoza msomaji katika kazi ya kifasihi. Rowe (1939:26) ameifasiri ploti kama:

Mfululizo wa matukio ambayo yamepangwa kwa jinsi ambayo itaweza kuimudu makini ya msomaji kwa kuwa na tataruki. Ploti ndiyo hutumiwa katika kusimulia hadithi.

Kwa hivyo kulingana naye, bila ploti hadithi haiwezi kusimuliwa. Rowe anaendela kusema kuwa ploti ndiyo nyenzo ya kuwasilishia mada ya kifasihi kwa hadhira.

Wamitila (2000:142) anasema:

Ploti ni mpangilio wa matukio yanayopatikana katika hadithi na kuhusisha matendo ya nguli na jinsi yanavyoathiri wahusika wengine. Ploti hueleža jinsi matukio hayo yanavyofuatana kwa kuzingatia visababishi vyake.

Perrine (1959:58) ametoa maelezo yake kuhusu ploti.

Amesema:

Ploti ni mpangilio wa vitushi ambavyo hujenga kisa. Ploti ni kama ramani inayotumiwa katika safari.

Anaendelea kusema kuwa:

Ploti ni utaratibu wenye kupendeza unaotokana na ile hali ya kufuata pamoja na kushiriki katika matukio ya kidhahania yanayotokana na umbuji wa mtunzi wa kisanaa.

Mazrui na Syambo (1992:97) wanasema kuwa, katika kuipanga ploti, mwandishi huwa anajaribu kuwavutia wasomaji wake kwa kuyafanya matukio yadhihirishe mgongano wa aina fulani. Wamesema kuwa, ploti nzuri yapaswa kuwa na taharuki. Kwa jumla, ploti ni mojawapo ya vijenzi vya kazi ya kidrama ambavyo huitawala kazi hiyo kuanzia mwanzo hadi mwisho. Ploti ni mbinu fiche ambayo hujidhihirisha katika mtazamo wa kijumla wa mpangilio na uhusiano wa vipengele mbalimbali vyenye kuijenga kazi fulani ya kisanaa.

Kuna matazamio ya ploti inayofaaa. Mtaalam Highsmith (1972:33) amesema kuwa, mtunzi apaswa kutokea na ploti yenyenye mantiki ambayo hubeba uhalisia katika kisa kinachoelezwa. Ploti hujengwa na wahusika kwa vile, bila wao hakutakuwa na matukio. Wao ndio hutenda katika kazi ya kifasihi na kutenda huko ndiko huendelea kuimarika kulingana na hatua za uendelezaji wa kisa hicho. Kwa hivyo, ploti lazima ionekane ikikua na kuimarika kulingana na jinsi visa vinavyoendelea.

Ploti inahusishwa na mgogoro. Rowe (1939:27) anasema mgogoro ni ule mvutano wa nguvu mbili zinazopingana na matokeo yake yakiwa hayaeleweki. Wamitila (2003:121) amefasili mgogoro kama mvutano unaokuwako kati ya mhusika mmoja na mwingine au katika akili ya mhusika mmoja na huwa sehemu muhimu ya msuko (ploti). Anaendelea kusema kuwa, bila mgogoro, ploti itakwama.

Rowe (1939:27) anasema mgogoro mzuri wapaswa uwe kati ya nguvu mbili ambazo zipo karibu sawa kwa vile, zikiwa sawa kutatokea mtanziko na hivyo kukwamiza ploti isiweze kuendelea mbele. Mgogoro usiwe pale ambapo upande mmoja una nguvu sana zaidi ya mwingine. Kwa vile hali kama hii ikitokea, hakutakuwa na hamu ya msomaji kutaka kuendelea na kusoma hadithi. Anasema kuwa, chanzo cha mgogoro kiwe ni vikwazo tosha.

Vikwazo kulingana na Rowe (1939:28), ni hali yoyote mpya ambayo huingia baada ya hadithi kuanza na ambayo huathiri mwelekeo wa mgogoro. Packard (1997:45) anasema kuwa, kikwazo ni chochote kile ambacho husimama kati ya mhusika na kile ambacho anakitaka, yaani lengo lake. Anapo jibidiisha katika kukabiliana na kikwazo hiki, ploti inasonga mbele. Kwa kuwa na vikwazo vingi, ploti huimarika kwa vile, kunatokea taharuki. Kwa hivyo, ploti nzuri lazima iwe na taharuki. Wamiti la (2003:212) anasema taharuki ni ile hamu kubwa anayokuwa nayo msomaji katika kutaka kujua yatakayotokea katika hadithi fulani .

Syambo na Mazrui (1992:78) wanasema kuwa, taharuki huwa kubwa zaidi iwapo msomaji hajui kabisa mambo yanayofuata. Ploti huwa ina matarajio, mshangao na mliwazo. Matarajio hutokea wakati wahusika wanapowekwa katika hali fulani ambayo humfanya msomaji atarajiye kuwa kitendo fulani kitatokea. Mambo yakienda kinyume na matarajio, kunatokea mshangao. Ikiwa yatatokea kulingana na matarajio, kuna kuwa na mliwazo.

Kwa jumla twaona kuwa, ploti hujengwa na vikwazo na migogoro na huimariswa na taharuki. Ploti inayofaa ni ile yenyé mshikamano wa migogoro iliyo na vikwanzo vyá kutosha vyá kujenga upeo. Ploti hiyo huwa kama wimbi zuri linavyozuka, kukua na kuimarika baharini mpaka linapovunjika kaktika ufuo wa bahari. Hivyo, ploti yapaswa iwe yenyé mshikamano wenye kuashiria umoja unaojengwa na vitushi vyá kisa katika mfuatano wenye mantiki. Rowe (1939:32) anasema kuwa, ploti nzuri haipaswi kuanza au kumalizika shaghlabaghala.

2.02 PLOTI KATIKA WINGU LA KUPITA

Tamthilia ya *Wingu La Kupita* imegawanywa katika matendo sita. Tendo la kwanza lina maonyesho mawili, la pili onyesho moja, la tatu maonyesho mawili, la nne mawili, la tano maonyesho matatu na tendo la mwisho lina maonyesho mawili.

Katika tamthilia hii, kisa kinaanza pale ambapo mhusika Mama yumo nyumbani akiwa ameanika nafaka juu ya mkeka ili zipate kukauka. Watoto wake wawili wanaingia kutoka shulenii na baada ya mazungumzo na mama yao, wanataka kujua kama baba yao anaishi juu mawinguni ambayo yanaliziba jua na kuzifanya nafaka zisikauke haraka. Mama watoto analipuuza swali hilo lakini watoto wanasisitiza kuwa waliambiwa na mwalimu wao wawaulize wazazi wao maswali ikiwa wanayo. Hapa kunazuka mgogoro kati ya mama na watoto ambapo watoto watashikilia kuwa baba na mama ni sawa ilhali mama ashikilia wao ni tofauti. Hali hii inazua taharuki kwa msomaji ya kutaka kujua mambo yataendelea vipi.

Ni katika sehemu hii ambapo watoto wanamjulisha mama yao kuwa walijua kuwa baba yao halisi alikufa mwaka uliotangulia. Jambo hili liliendelea kuimarishe mgogoro kati yao lakini mtunzi anausuluhisha kwa kuyakatiza mazungumzo hayo kimakusudi. Kisa kinachukuwa mwelekeo mwingine baada ya Mama kuwaauliza walichofundishwa shulen na wao wakamjibu kuwa walifunzwa wimbo mpya wa Wingu la kupita. Swali hili la mama lilisababisha kuimbwa kwa wimbo na watoto wake. Lakini ukosefu wa wizani katika wimbo ukasababisha kutofurahiwa kwa wimbo na mama.

Baada ya kisa hiki cha watoto kuimba wimbo, walimuomba mama yao awatambe hadithi ili waitambe siku iliyofuata shulen mwao. Mama aliwatambia hadithi juu ya ndovu na chura. Hadithi hii inamfanya msomaji kuwa na taharuki ya kutaka kujua kitakachotokea kati ya chura na ndovu. Mwishoni mwa onyesho hili msomaji anaachwa na taharuki ya kutaka kujua alipoondoka kwenda Mama. Inaonekana kuwa kuna mambo mengi yaliotendeka baada ya Mama kuondoka. Kwani aliporejea ni siku nyingine ya pili alipotoka kutafuta kuni. Kisa kinachoendela ni cha mama kuingia na kuutuwa mzigo wa kuni. Taharuki ya msomaji inaimarishwa kwa kutaka kujua kinachosababisha baba kuondoka nyumbani kila wakati na huwa akienda wapi.

Mara watoto waliingia kutoka shulen wakiimba wimbo ule ule wa Wingu la kupita. Walipoingia walianza kulia njaa na mara wakataka kujua alipo baba yao ili wamjulish juu ya vitu walivyovitaka kutoka kwake k.m sare za shule, kalamu na vitabu. Licha ya kuwa hakai nyumbani, Baba hawajali watoto wake, kwani alikuwa amekila chakula cha watoto kilichobaki kabla ya kuondoka. Kutokama na ukosefu wa chakula, Mama

aliwaomba watoto waende kwa Michonge wakaombe chakula. Lakini watoto wakakataa wakiogopa kuchekwa na majirani zao. Jambo hili lilizusha mgogoro baina ya Mama na watoto kwani watoto waliona ni vibaya kwenda kuomba chakula. Mgogoro unasuluuhishwa kwa sauti kusikika nje na wote wakataka kujua ilikuwa ya nani.

Sauti hii ilianzisha mgogoro mwingine ambapo mvulana alishikilia kuwa ni ya jirani yao Michonge na Msichana kushikilia kuwa ni ya baba yao. Maongezi yaliyoendelea ni baina ya mama na sauti. Lakini kukawa na ukinzano wa kimawazo baina ya sauti na mama juu ya chanzo cha maafa yao ya njaa. Sauti ilishikilia kuwa, asili ya hali hii ni ukosefu wa azimio na sera lakini mama alishikilia kuwa azimio hazina maana katika kuleta chakula.

Ni baada ya maongezi haya baina ya Mama na sauti ambapo watoto walikumbuka kuwa walibakisha maboga asubuhi lakini baba yao alikuwa ameyala. Kitendo hiki kilipelekea Msichana kumkana baba yao. Onyesho linaisha kwa watoto kurudia wimbo wao.

Tukio lililofuata ni la Mama kusaga unga huku akiimba lakini ghafla mwanamke aliingia akiwa na ujumbe kuwa kulikuwa na mkutano shuleni lakini wao hawakuhudhuria. Mumewe mwanamke alihudhuria kwa niaba yake lakini hakuna aliyehudhuria kutoka kwa mama. Baada ya muda tu mwanamke alimfahamisha Mama kuwa alikutana na Baba akielekeea kwenye njia isemwayo kuwa ina majini.

Mwanamke huyu anaongeza tataruki yetu ya kutaka kujua mahali halisi ambapo Baba alikuwa akienda. Hali hii ya kutotulia nyumbani kwa baba ilimpelekea Mama kutaka kujua kile mwanamke alichompa mumewe ili aweze kumtii. Mama alitakakuja hili ili

naye ampe wake. Lakini mwanamke aliona kheri mumewe Mama aondokaye nyumbani kuliko wake ambaya hukaa nyumbani kila wakati.

Kwa kutumia mbinu rejeshi, Mwanamke anatujulisha mumewe alivyokuwa kabla ya kuchukuliwa hatua na Mama naye anatujulisha yaliyotokea mpaka akaolewa na bwanake wa sasa. Mtunzi anayabadilisha mandhari kutoka nyumbani hadi katika hali ya ufungwa ambapo tunakutana na Jaribosi na mfungwa mwenzake. Msomaji anadokezewa sababu ya kufungwa kwao. Ingawa wote walifungwa, mwenzake Jaribosi alifungwa kwa kushiriki katika wizi ambapo Jaribosi alifungwa kwa kuzuia wizi wa mali ya umma na viongozi serikalini ambapo naye mwenzake, aliyekuwa mkuu serikalini, alifungwa ili kuwafumba raia macho kuwa hata serikali haiungi mkono wizi huo. Kuna mgogoro wa kimawazo baina ya Jaribosi na mwezake juu ya mtazamo wao wa wizi wa mali ya umma.

Kwa kutumia mbinu rejeshi, mwandishi anatujulisha yaliyosababisha kufungwa kwa Joribosi. Kilichosababisha mawazo ya Joribosi ni yale mazungumzo baina yake na mfungwa mwenzake hapo mbeleni. Mtunzi anabgilisha mazingira ya jera na kuturundisha katika mazingira ya nyumbani tunapokutana na Mama na watoto wake. Watoto walingia kutoka shule na kuanza kulalamika kuwa, vitabu vyao vilichukuliwa na shule yao kwa vile havifai kutumiwa na badala yake vitaandikwa vipyta vitakavyokosoa makosa ya vile vyaa zamani.

Katika onyesho linalofuata mtunzi anatujulisha kuwa uhusiano kati ya familia ya Baba na Michombe siyo mzuri kiasi kwamba siku hizi watoto wa familia hizi mbili hawali pamoja sababu ikiwa kwamba Baba hataki wale pamoja. Ingawa hivyo, mtunzi anatuacha

katika hali ya taharuki ya kutaka kujua sababu ya baba kutotaka washirikiane. Katika sehemu hii ni hapa ambapo tunajulishwa kuwa baba alikuwa mwalimu mbeleni, lakini msomaji anaachiwa na taharuki ya kutaka kujua kilichomfanya aache ualimu.

Mtunzi, kwa kutumia sadfa anawakutanisha Mama na Mwanamke kisimani na katika mazungumzo yao wakatujulisha kuwa Michonge alikuwa radhi kutwaa uongozi kwa vile alikuwa ameshindwa nao. Ni hapo Mama alisema kuwa kila mtu ana matatizo, ye ye akiwemo.

Maongezi yanayoendelea ni juu ya jinsi Jaribosi alivyoupinga uhusiano baina ya Baba na Mama. Kisa hiki cha kuwa kisimani kinafuatwa moja kwa moja, kama ilivyo katika hali halisi, na kile cha Mama kurudi nyumbani kwake. Baadaye alitaka kujua kama watoto walikuwa wamekwenda kwa mhubiri alikokuwa amewatuma. Ingawa Mama aliwauliza habari za kwenda kwa mhubiri, hapo mbeleni kabla ya kwenda kisimani (uk. 43), watoto walikuwa wamekwenda malishoni na siyo kwa mhubiri.

Kwa hivyo kuna ukosefu wa mantiki katika mambo haya. Ingawa hivyo, tumeweza kujua kuwa mumewe huenda kwa mhumbiri mara nyingi. Tunaachwa tukishangaa ni kwa nini Baba awe akienda kwa mhumbiri mara nyingi. Baada ya watoto kurudi, walimjulisha mama yao kuwa Baba awehulu kwenda kwa mhubiri. Tungetarajia Mama akasirike kwa kundanganywa na Baba na wanapokutana tena amwulize aendapo. Lakini hili hatulioni likitendeka katika tamthilia hivyo tunaachwa na mshangao.

Katika onyesho la tatu tendo la tano, tunakutana na Jaribosi na Mfungwa tena katila jela. Jaribosi yu karibu kuondoka jela. Wanakubaliana katika maongezi yao kuwa dhuluma itaisha kwa kuikabili dhuluma na nyingine. Matukio ya tendo la mwisho ni pale kijijini.

Mvulana ametoka shuleni huku akimwacha dada yake nyuma. Mtoto huyo alimjulisha mamake kuwa mwalimu wao aliywafundisha wimbo wa wingu alikuwa ameondoka na hangerudi shuleni na kuwa walijulishwa hili na mjukuu wake Kalimao.

Ni baada ya tukio hili ambapo kulitokea sauti ambayo haikujulikana ni ya nani. Msomaji anatiwa taharuki ya kutaka kujua sauti hiyo ni ya nani. Wakati huo huo kunasikika sauti chumbani lakini mama anatujilisha haraka kuwa ni ya bwanake (Baba). Ploti inaenda kwa kasi kutoka pale tunapokutana na Jaribosi akiwa karibu kuondoka jela kwani kisa kinachofuata ni pale ambapo tunakutana naye akirudi nyumbani. Kwa sadfa akapatana na nduguye Msichana akiwa amepigwa na askari wa chifu. Wote wawili wakaenda nyumbani na baada ya kufika nyumbani walimkuta mama yao hapo. Mara alipowaona watoto wake akaingiwa na huruma kwa hali waliyokuwa nayo. Mama alishangaa kwa nini askari wampige mtoto wa umri mdogo hivyo. Tamthlia inapokamilika tunamwona Mama akikubaliana na Jaribosi kuwa baba si mwema na ndiye aliye kama wingu ambalo litapita kwa hivyo tamthlia ina kuwa tamthlia ungamo.

2.03 TATHMINI

Wingu La Kupita ni tamthilia ambayo mtunzi hajaweka mgogoro wa kutosha ili iwe na taharuki nzuri. Rowe (1939;27) anasema kuwa, mgogoro mzuri wapaswa uwe kati ya nguvu mbili ambazo zipo karibu sawa. Katika tamthilia hii hakuna nguvu mbili zinazopingana kwa vile tuna upande mmoja tu, yaani wa mhusika Mama. Lakini mhusika mwingine ambaye angeleta ukinzano huo ni Baba ambaye anatajwa tu bila kujitokeza dhahiri katika tamthilia nzima.

Kama mtunzi angemfanya mhusika Baba ajitokeze na kutenda katika tamthilia, mgogoro ungeimarika na kukua vizuri kwa vile baba angekuwa akipingana na mawazo na vitendo vyta Mama. Hivyo kuisukuma hadithi mbele. Pengine Baba angekuwa akijitetea dhidi ya shtuma zinazotolewa na Mama dhidi yake. Mtunzi amemfanya Baba kutotokea kila wakati na hivyo kuondoa mgogoro ambao ungeifanya tataruki iwe yenye nguvu.

Kuna mambo ambayo hayana mantiki katika tamthilia hii. Kwa mfano, katika ukurasa wa kwanza, mtunzi anatudokezea kuwa, umri wa Mvulana ni miaka kama sita hivi na katika orodha ya wahusika amesema kuwa yule Msichana ndiye mkubwa kiumri kuliko mvulana, hivyo, huyu Msichana ana umri wa miaka minane au zaīdi. Katika ukurasa wa pili, Msichana huyu anasema kuwa ndugu yao Jaribosi ndiye aliyewajulisha kuwa baba yao halisi alikuwa amefariki mwaka uliotangulia. Katika hali halisi, mtoto wa miaka saba huwa na ufahamu wa kutosha kuelewa kuwa mzazi amekufa. Dai hili la msichana kwamba baba yao alikuwa amekufa mwaka uliotangulia linapingana na lile la mama katika (uk 19). Katika (uk. 19) Mama aliyakumbuka mambo yāliyofanyika kabla ya mumewe wa kwanza kufa. Katika ukurasa huo alisema hivi: '*zamañi walifika watu kwetu* ikiwa tunaarifiwa kuwa mumewe huyo wa kwanza aliaga mwaka uliotangulia basi Mama huyu hangetumia neno zamani kwani mwaka uliotangulia sio zamani.

Mama ametoa sababu ya kukubali kuolewa na mumewe wa pili kuwa ni ile hali ya kutaka kujua walipopelekwa wanawe na wale wapora ng'ombe. Lakini katika (uk.45) alielezea

kuwa sababu iliyomfanya akubali kuolewa ni kwa kuwa watoto wake walikuwa wamemfahamu na kumzoea huyo bwanake wa pili.

Maelezo haya yanapingana na kumfanya msomaji kushindwa kuelewa sababu halisi iliyomfanya akubali kuolewa. Mambo haya yanaifanya ploti na wahusika wasiwe wa kukubalika. Rowe, (1939; 152) anasema kuwa mtunzi hutazamiwa kuwaumba wahusika na ploti kwa jumla kwa njia inayoweza kukubalika. Hivyo, jambo hili linaivunja ile kaida ya ukubalifu wa ploti. Kuna mambo mengine ambayo hayana uhalisia katika tamthilia na yanaifanya ionekane kuwa ya ajabu na hivyo kutokubalika vizuri akitini mwa msomaji.

Baada ya Mama kuwa kisimani na Mwanamke, kisa kinachofuata ni cha Mama kurudi na kufika nyumbani. Ingefaa kama mtunzi angeweza kuwaondoa wanawake hawa wawili kisimani na waandamane mpaka mahali fulani halafu waachane ili Mama afike nyumbani kwake. Haieleweki kama yule mama aliachwa kisimani au aliondoka kwani hili halijitokezi katika tamthilia. Wakati Mama alipokuwa akizungumza na sauti ambayo hajui asili yake, haonyeshi kushangaa na hata watoto wake walikaa wakimtazama alipokuwa akizungumza na sauti hiyo. Katika hali halisi tungetarajia Mama na watoto hawa wapatwe na uoga na hivyo wasiweze kukaa wakiisikiliza sauti hiyo.

Hata ingawa mtuo ni njia moja ya kujenga tataruki, mtunzi ameitumia sana katika tamthilia yake na hivyo kumfanya msomaji achoshwe nayo. Msomaji anaitarajia kila anapoisoma tamthilia hii. Kuhusu kitendo kama hiki, Rowe anasema:

Msanii hupaswa kuwaumba wahusika na kuisawiri ploti kwa njia ambayo kila mhusika na kila tukio linadhihirisha ukweli kama unavyotokea katika jamii. Jinsi watu walivyo hutambulikana kutokana na matendo yao wakati wanapokabiriwa na matukio ya dharura. (uk. 102)

Katika onyesho la kwanza Mama na watoto wake walikuwa nyumbani baada ya watoto kutoka shuleni na kumwomba mama yao awatabie hadithi. Baadaye, Mama aliondoka kwenda kutafuta kuni. Aliporudi, watoto nao walirudi kutoka shule. Kwa vile aliwaacha nyumbani na hawakurudi shuleni, tunachukulia kwamba, Mama alipotoka kutafuta kuni na wao kurudi nyumbani kutoka shule, ilikuwa siku iliyofuata. Inaonekana kuwa Mama alitumia usiku mzima kutafuta kuni. Kitendo hiki hakiaminiki kwa vile mtu hatafuti kuni usiku mzima.

Kisa kingine ambapo mambo hayaeleweki ni wakati Jaribosi alipoingia akiandamana na nduguye Msichana. Mvulana ambaye tayari alikuwa amefika nyumbani kabla ya Msichana, ndiye aliyeingia kumfahamisha mamake juu ya kupigwa kwa nduguye Msichana. Wakati alipoingia mara ya kwanza, hakutoa habari hizo kwa mamake. Haieleweki ni vipi aliondoka nyumbani na kumpata dadake akiwa amepigwa na askari. Hata tukio la askari kumpiga mtoto wa umri mdogo kwa sababu alikuwa ameandamana na mwalimu wao ni jambo lisilo na uhalisia.

Baada ya Jaribosi kurudi nyumbani kutoka kifungoni, alikutana kisadfa na nduguye (Msichana) ambaye alikuwa amepigwa na askari na wakaandamana hadi nyumbani. Baada ya kufika nyumbani, Mama hakumlaki Jaribosi kwa furaha. Inashangaza kwa vile msomaji anatarajia Mama afurahie kurudi kwa mwanawe kutoka kifungoni. Tukio hili linaonekana kama lililopachikwa na mtunzi ili tamthilia ichukue mkondo alioutaka. Kuhusu tukio kama hili Syambo na Mazrui (1992: 95) wanasema kuwa:

Tukio lisilo na sababu kupachikwa tu hadithini ili ploti iendelee au imalizike vile mtunzi anavyotaka huifanya tamthilia iwe chapwa

Taharuki ya msomaji kutaka kujua sababu za baba kutotulia nyumbani haimalizwi hata wakati tamthilia inapomalizika. Msomaji anaachwa pia akitaka kujua baba huyu huenda wapi kila anapoondoka nyumbani. Ingefaa mtunzi ayajibu maswali haya katika tamthilia yake.

Tamthilia inamalizika kwa kuning'inia ambapo msomaji anaachwa akijiuliza kama Mama aliachana na Baba au la baada ya kukubali kuwa alikuwa (Mama) mjinga siku zote zile waliishi naye. Haieleweki kama walisuluhisha matatizo na kuishi pamoja. Ingawa kuna udhaifu katika ploti, mtunzi ameweza kudhibiti vipengele tofauti vya ploti katika baadhi ya sehemu za tamthilia. Kwa mfano, ambapo Jaribosi alikuwa akizungumza na mwenzake katika jela. Kuna taharuki na mgogoro. Pia ameweza kutumia mbinu rejeshi katika kuelezea sababu za matukio kadhaa. Kwa mfano, pale ambapo Mama anakumbuka kilichomfanya aolewe na bwanake wa pili na kilichosababisha kufungwa kwa Jaribosi. Ametumia hadithi katika kuendeleza mawazo yake. Mbinu hizi zinaifanya tamthilia hii iwe na uchangamano katika kuijenga ploti.

2.04 PLOTI KATIKA PANGO

Tamthilia ya Pango inaangazia utata wa kisiasa, uchumi, uongozi na migongano ya wimbi la ukale na la usasa. Hadithi inawazunguka wahusika wawili; Katango na Ngwese. Ngwese ni mzee ambaye ni tajiri katika sehemu ya Pango nchini Chemwa naye Katango ni msichana ambaye amesoma na sasa ni mwalimu.

Tamthilia inaanza na mgogoro baina ya Ngwese na watoto; Susa na Sota ambao ni ndugu. Watoto hawa walikuwa katika safari ya kwenda kisimani kuteka maji. Lakini baada ya kuingia shambani mwa Ngwese, ambapo kisima kimo, Ngwese alitokea na kuwakataza kwenda kuteka maji. Watoto walimsihi awaruhusu kwenda kisimani lakini kwa ukali aliwakataza licha ya kumsihi.

Makelele baina ya watoto na Ngwese yalisababisha kuingia kwa Sakina mkewe Ngwese na mara alitaka kujua sababu za makelele yale baina ya Ngwese na watoto. Mazungumzo baina ya Ngwese na mkewe Sakina, yanaonyesha mgongano wa kimawazo baina yao. Sakina alishikilia kuwa, watoto wapaswa kuruhusiwa kuyateka maji ambapo Ngwese aliona maji ni yake ni hivyo hayangetekwa na watu wengine. Mgogoro unasuluuhishwa kwa kuondoka kwa Sakina na kumwacha Ngwese akijizungumzia.

Kisa kinachofuata ni cha Ngwese kuonana na Katango. Maongezi yalioendelea kati yao yanadhihirisha mgogoro wa uadui uliopo baina yao. Katango ălimjulisha Ngwese kuwa tayari alikuwa amemwona Ngwese akiwakataza Susa na Sota kwenda kisimani na kuwafukuza kama ndege. Ngwese alikana, na kusema huo ulikuwa uzushi wa Katango. Maongezi yaliyoendelea kati yao yanaonyesha jinsi Ngwese alivyo na

taasubi ya kiume kwani anamwambia katango kuwa "*mwanamke ni mwanamke tu*"! (uk. 10). Kitendo hiki kinazusha mgogoro kati yao ambapo anakuzza tahaaruki ya msomaji kutaka kujua jinsi Katango atakavyojibu kwa kutusiwaa.

Kupitia kisa kilichofuata tunajulishwa kuwa, Katango alikuwa ameona dada zake wakifukuzwa na kukatazwa kwenda kuteka maji kisimani na Ngwese. Na hivyo, walipokutana wakaanza ugomvi juu ya kitendo hicho kibaya cha Ngwese. Ngwese alimjulisha Katango azma yake (Ngwese) kutaka kuwa kiongozi wa Pango ambapo naye Katango alimwalifu Ngwese kuwa hata yeze ana azma hiyo hiyo. Kwa hivyo, mtunzi anatundokezea kitendo cha kila mmoja: yaani kuwa kiongozi. Lengo hili la kila mmoja kutaka kuwa kiongozi ndilo linalo sababisha ushindani kati yao. Mgogoro wa tamthilia nzima unatokana na azma hii.

Hadithi inasonga mbele moja kwa moja na watoto wanarudi nyumbani kutoka kisimani lakini wakiwa wamechelewa – kulingana na mama yao. Watoto walimweleza mama yao kilichowafanya wakawie lakini mara Katango aliingia na kuunga mkono sababu zao za kuchelewa. Mtunzi kwa haraka anamwingiza Seki-baba yao Katango na watoto. Seki alimtetea kinaleta mshangao kwa msomaji kwani tayari imendokezwa hapo mbeleni Ngwese alikuwa amefunga hivyo. Msomaji anaachwa na tahaaruki ya kutaka kujua sababu ya Seki kumtetea Ngwese. Hata baada ya Katango kumjulisha babake kuwa anataka kuwania uongozi wa Pango, Seki alimvunja moyo badala ya kumhimiza aendelee na azma hiyo.

Mgogoro unazuka baina ya Seki na bintiye Katango juu ya utamanduni kwa vile Katango alikuwa ametenda kinyume cha utamaduni kwa kubeba mishale na uta.

Kitendo ambacho hakikuwa kifanywe na wanawake katika jamii hii na pia Katango aligoma kushiriki tohara. Kulingana na Katango mambo haya hayana maana kwa vile mambo yamebadilika.

Matukio yanayofuata yanatendeka pale hotelini ambapo tunakutana na vijana ambao wanajadaliana juu ya habari zilizokuwa gazetini zilizosema kuwa, Katango alitaka kuchaguliwa kuwa kiongozi wa Pango. Kunazuka mgogoro baina ya vijana hawa ambapo upande mmoja unaunga mkono jambo hilo na mwingine kulipinga. Mara ghafla Katango aliingia akiwa na ndugu zake wale wawili – Susa na Sota – na mara akaingia katika mjadala wa wale vijana juu ya uongozi huku akitetea sababu zake za kutaka kuiongoza Pango. Kisadfa Ngwese na watu wengine wawili waliingia na Ngwese kuanza mazungumzo na Kauleni ambaye ndiye mwenye hoteli. Kisa cha Ngwese kuwa mahali pamoja na adui yake kwa wakati mmoja kinaleta tataruki kwa msomaji kwa kutaka kujua watakabiliana vipi.

Tataruki hii inaondolewa haraka kwani katango na Kibwana wanaondolewa na mtunzi mle hotelini bila kuonana na Ngwese. Baada ya Katango na Kibwana kuondoka hotelini walifuatwa na watu wale waliokuwa pamojua na Ngwese na mara watu hao wakawashambulia pamoja na Kibwana. Kwa haraka Susa alijitokeza na kumpiga mmoja wa wale wawili kwa yai na hapo vita vikaisha.

Kwa haraka hadithi inabadilika na kutupeleka ambapo, kundi la vijana lililombeba Katango lilitokea huku likimsifu kwa njia ya wimbo. Kundi lingine lililombeba Ngwese nalo liliingia huku likimsifu kwa wimbo. Kwa vile tayari mtunzi ametuonyesha hali ya uadui kati ya Katango na Ngwese, matarajio yanayoibushwa ni kuwa, patatokea vita au ugomvi kati ya makundi haya mawili. Lakini kinyume na matarajio hayo, vita au ugomvi havikutokea hivyo msomaji anaachwa na mshangao

wa kwa nini wasigombane ilhali uadui wao ni dhahiri na ni wa hali ya juu. Kwa mgogoro baina ya kundi la ngwese na Katango

Mara babu kuyaongoza makundi haya mawili na akatoa nafasi kwa kila mmoja alimpa Katango nafasi ya kwanza ya kujitetea mbele ya umati na kisha akatoa nafasi kwa Ngwese. Kila mmoja alijitahidi kujitetea na baadaye uchanguzi ulifanywa kwa haraka na Ngwese akamshinda Katango. Hapa basi ploti inafika upeo wa juu.

Baada ya uchaguzi, kila mmoja-Ngwese na Katango – alirudi nyumbani. Nyumbani kwa Ngwese tunakutana na bibiye Sakina akimhiza aende kazini lakini Ngwese aliendelea na kusoma gazeti lililokuwa na habari za ushindi wake. Kauleni na Ngoi waliingia wakati huo kwake Ngwese na kumsifu kwa ushindi wake. Namo nyumbani kwa Katango hakukuwa na furaha. Katango alikuwa akiomboleza kushindwa kwake. Lakini babu na mama walikuwa wakimliwaza Katango kwa kushindwa.

Mara waliingia Kibwana na Kikubi - marafiki zake Katango – ambao walimjulisha Katango kuwa kulikuwa na mchezo mle pangoni unaochezwa na Susa na Sota.

Katango, Kibwana na Kibubi waliondoka kwenda pangoni kuhakikisha kama ni Susa na Sota waliokuwa wakicheza mle pangoni. Sehemu iliyofuata ni karibu na pango ambapo palikuwa na mtu aliyelala na kujizungumzia. Mara Susa na Sota wakaingia pale karibu na pango na wakaona kuwa, aliyekuwepo pale ni dada yao Katango. Ni hapo walipoamua kwenda kumjulisha babu yao ni nani hucheza pangoni. Walimwambia ni dada yao Katango na wakamjulisha jinsi alivyokuwa haqnegei na kuwa alikuwa akijaribu kutoroka lakini alikuwa anashindwa. Hali hii ya Katango

inatia tħaruki katika ploti kwani msomaji angetaka kujua kilichosababisha kutoongea na kutaka kutoroka kwa Katango.

Ni wakati huu ambapo baba yao (Seki) alitokezea na kushikilia kuwa, Susa na Sota walicheza pale pangoni na hivyo kumfanya akaaye kisimani kulalamika. Baadaye Susa na Sota walimjulisha aliyecheza kisimani ni Katango. Hili lilimfurahisha baba yao sana. Ni wakati huo alipokuwa akifurahi ambapo Katango aliingia na kukaa bila kuongea na kisha akaondoka.

Kilichofuatia ni kisa ambapo Susa na Sota wamo mbele ya pango na sauti ikatokea humo pangoni. Kisa hiki kinakuza tħaruki kwa msomaji cha kutaka kujua āsili ya sauti. Mara Susa na Sota waliona sarafu na kikaratasi kilichokwuwa na maandishi ya ajabu. Ni wakati huu ambapo sauti iliyowatisha ilitokea. Sauti hiyo iliongea juu ya maua na asali. Mara wakapanga kuondoka kwenda kumjulisha baba yao kuwa walimwona aliyevuruga pango. Lakini wakaogopa kuwa baba yao hangewaamini.

Hadithi ilioendelea ni pale pangoni ambapo palisikika sauti ya bundi na ya jogoo. Kulikuwa na majitu matatu na kunatokea mkinzano wa kimawazo baina ya jitu la kwanza na la pili juu ya ishara za kulia kwa yule ndege bundi. Jitu la kwanza lilichukulia kuwa, hiyo ni ishara mbaya na la pili likasema huyu ni ndegé mzuri ambaye hulishwa na watu huku kwao.

Jitu la kwanza lilikuwa na msimamo kuwa wangelifilisi pango baada ya kuchukua kila kitu na kuhamishia ughaibuni. Lakini walimwogopa mwalimu asije akapinga hili.

Waliona njia ya kumnyamazisha ni kwa kutumia pesa wamhonge. Ni baada ya tukio hilo ambapo walitokea Katango, Kibwana, Mama, Sota, Susa na Babu.

Sauti zao zililetu wasiwasi kwa yale majitu. Mara wanakijiji waliingia na baada ya muda Katango akafunua yale majitu na watu wakashangaa kuona mmoja wa majitu yale ni Ngwese, la pili ni Seki lakini la tatu halijulikani. Tunaweza kukisia kuwa ni Ngoi kwani ni rafikiye Ngwese. Mwishoni mwa tamthilia, wanaingia polisi wawili walioandamana na Mbabekazi na kumshika Ngwese kwa kuwa, alikuwa amefuja mali ya umma alipokuwa Mkurugenzi. Kisa hiki cha kushikwa kwa Ngwese ambapo kilitoa mwanya wa uongozi kwake Katango bila yeche Katango kusumbuka tena.

2.05 TATHMINI

Kisa katika *Pango* kinawazunguka wahusika wakuu wawili: Ngwese na Katango. Mtunzi ameweza kubainisha mwanzoni mwa tamthlia kitendo cha kila mmoja wao: yaani kutaka kuchaguliwa kuwa kiongozi wa *Pango*. Katika (uk.8) Ngese alibainisha azma yake hiyo na katika ukurasa wa kumi na moja Katango naye alitubainishia lengo hilo. Kwa hivyo, wote wawili wana lengo moja ambalo ndilo walishindania katika tamthilia nzima. Hivyo kila mmoja akawa mpinzani wa mwingine.

Matukio ya ploti yanajenga tataruki ya msomaji kutaka kujua jinsi mambo yatakavyoendelea wakati wa kugobania uongozi huo na ni nani atakaye kuwa mshindi mwichoni.

Mtunzi amefaulu katika kubainisha motisha ya kila mmoja wao. Kwani kutaka kuwa kiongozi ndiko kunakomotisha matendo ya kila mmoja wao. Ingawa mtunzi ameweza kubainisha chanzo cha mgogoro katika tamthilia hii, hajaifanya kuwa na nguvu zaidi

za kujenga tataruki yenyenye nguvu kwa msomaji. Kwa vile tamthilia hii ni ya hivi karibuni, (2003) tungetarajia kampeni za kuchukuwa uongozi zioane na zile ambazo tunazijua ambapo washindani huandaa mikutano ya siasa na kila mmoja humshambulia mwenzake kwa kutaja udhaifu wake huku yeye akijisifu. Huwa kuna matumizi ya vyombo vyanya kupitishia ujumbe wao kama vile: karatasi zenye picha zao na maandiko na pia vipasa sauti.

Wagombea uchaguzi huwa na ushindani mkali sana lakini siyo kama ilivyo hapa ambapo wagombea uchaguzi wanakutana tu wakiwa wawili pekee yao na kuanza kushambuliana kwa matusi.

Tunapoendelea na ushindani wao wa uongozi, tunaona kuwa uchaguzi ule ulifanywa kwa njia isiyo na mpango ambapo makundi mawili yalikutana – yaani la Katango na la Ngwese na mara mzee mmoja – Babu –alichukua nafasi ya kuendesha uchaguzi. Papo hapo uchaguzi ulifanywa baada ya muda mfupi kwa njia rahisi mno na watu wakamchagua Ngwese. Kitendo hiki hakikubaliki akilini mwa msomaji wa tamthilia hii kwani hakina uhalisia.

Haieleweki vipi watu wengi hivi wadanganywe kwa kutupiwa matunda na Ngwese ili wamuunge mkono. Kuhusu kitendo kama hiki Rowe (1939: 152) anasema:

Msanii hupaswa kuisawiri ploti kwa njia ambayo kila mhusika na kila tukio linadhihirisha ukweli kama unavyoweza kutokea katika jamii. Katika upande wa matukio kuna matendo ambayo hayaeleweki na yanayoonekana kuwa yamewekwa na mtunzi ili hadithi yake iende kama alivyotaka. Kwa mfano: Bwana Seki – babake Katango – kuwa aliingia wakati mazungumzo fulani yalikuwa

yanaendelea na akaweza kuyaingilia mara moja bila kuyatatiza kama mtu aliyekuwapo. Kwa mfano katika (uk. 17)

Mama: Mbona anawakata watoto maji?

Seki: Nani huyo aliywakataza watoto maji? Pia wakati Seki alipoingia kwa kishindo ambapo Babu alikuwa akiongea.

Babu: Asiwe karibu na pango?

Seki: Kwa nini hamfuati? (uk. 17).

Baada ya Katango na Ngwese kuondoka hotelini mwa Kauleni, kila mmoja aliingia na kundi la wafuasi wake na mara uchaguzi ukafanywa. Haieleweki ni vipi Katango na Ngwese waliwapata watu hao na kuja kukutana pamoja. Hakuna mahali popote tumeonyeshwa tarehe na mahali pao pa kufanyiwa uchaguzi. Basi walivyoyajua mambo haya haieleweki.

Jambo jingine ambalo halieleweki ni pale ambapo Katango aliingia nyumbani kwao baada ya kugombana na Ngwese akiwa na uta na mshale. Msomaji anaachwa akishangaa kwa nini Katango abebe uta na mshale na huku alikuwa akienda nyumbani kwao. Uta na mishale ingekuwa ya nini? Pia aliitoa wapi? Kitendo kingine ambacho kimetokea kisadfa ni pale Ngwese alikutana na Katango hotelini. Ingawa hawakuongea tunaona kuwa Ngwese alijua Katango yu hapo. Ni vigumu kuelewa vile Ngwese alikuja kujua Katango alikuwa hapo.

Wakati Katango na Kibwana walipopigwa na watu wale wawili njiani baada ya kuondoka hotelini, Susa na Sota walijitokeza na Susa akamshambulia mtu mmoja kwa yai. Haieleweki ni vipi hawa watoto wawili waliingia kwani hapo mbeleni katika (uk. 26) tumeelezwa kuwa baada ya kununuliwa mayai na mkate na dada yao Katango,

waliondokoka na kwenda nyumbani. Katango aliachwa hotelini akizungumza na wenzake kwa muda. Haieleweki ni vipi basi walikuja kutokea pale njiani baada ya kwenda nyumbani

Kitendo hiki cha pili hakina mantiki tukizingatia kile cha awali cha kuondoka kwao. Inaonekana mtunzi alikiingiza kitendo hiki cha pili ili kupata njia ya kusuluhisha ugomvi au vita baina ya pande mbili hizi. Tukio jingine ambapo mtunzi ameivunja kaida ya ukubalifu wa ploti ni pale mwishoni mwa tamthilia ambapo Mbambekazi alilingia na wale polisi wawili ambao walimshika Ngwese kwa uvujaji wa mali ya umma alipokuwa mkurugenzi katika shirika la umma.

Kuna kutoeleweka kwa vipi kijana huyu – Mbambekazi – alivyowapata hawa askari. Baada ya Ngwese kushikwa Katango alifanywa kuwa kiongozi wa Pango. Katika wakati wa sasa, uongozi hauwezi kupatikana kwa urahisi hivi. Mtunzi amekirahisisha kitendo hiki ambacho ni muhimu sana na kinachohitaji muda mwingi. Inaonekana amefanya hivi ili tamthilia imalizike kama alivyotaka yeye alipokuwa akitunga yaani iwe futuhi.

Kuna matukio mengine ambayo pia hayana ukubalifu. Kwa mfano: Susa na Sota ni watoto wa miaka michache tu yaani miaka kumi na kumi na mmoja. Hatutarajii watoto kama hawa wawe na ujasiri kama ule wa kusimama kusikiliza sauti za kutisha pale pangoni. Mtunzi anatuweka katika hali ya kutarajia wale watoto watoroke wakiwa na uoga mwingi tukizingatia umri wao. Lakini kinyume na matarajio, waliendela kukaa pale wakisikiliza yaliyokuwa yakisemwa na sauti wasiyojua asili yake. Kitendo hiki hakina uhalisia.

Tunaona pia kwamba, baada ya Katango, Kibwana na Kikubi kuondoka mle nyumbani mwa Katango kwenda pangoni kuchunguza juu ya madai kuwa Susa na Sota walikuwa wakicheza pangoni, haieleweki kama Kibwana na Kikubi walifika kule pangoni kwani yaliyofuata ni watoto kumkuta Katango pangoni akiwa amewekwa kitata kinywani. Tunaachwa tukijiuliza hawa wengine wawili walikwenda wapi na vipi sasa ikawa ni Kitango anayecheza ilhali hapo mbeleni Katango alipokuwa nyumbani kulikuwa na watu wakicheza pangoni.

2.06 HITIMISHO

Katika *Wingu La Kupita* na *Pango* mtunzi amejaribu kuzingatia baadhi ya vipengele vya ploti kama vile tataruki, mgogoro, mshangao, n.k. katika baadhi ya sehemu za kila moja ya tamthilia zake. Lakini twaona kuwa kuna baadhi ya matukio ambayo hayana ukubalifu wa ploti na pia mantiki.

Ameyarahisisha baadhi ya matukio sana kiasi kwamba hayakbaliki katika wakati wa sasa naametumia kaida kama vile ya mtuo sana katika tamthilia zote mbili na hivyo kushusha ploti yake kwa kurudiarudia hali hii sana. Ingawa hivyo, tunaona ya kuwa tamthilia ya pili yaani *Pango* inadhihirisha washindani wawili juu ya jambo moja-uongozi – kinyume na ilivyo katika tamthilia ya mwanzo *Wingu La Kupita* ambapo hakuna mgogoro kwani mhusika mkuu Baba hajitokezi hadharani.

SURA YA TATU

3.00 UMBUJI WA WAHUSIKA

3.01 UTANGULIZI

Uhusika ni mojawapo ya dhana muhimu ambazo hutawala utunzi wa kazi za fashihi. Mbatia, M. (2001: 96) ameeleza uhusika kama utratibu wa kuwaumba wahusika pamoja na kunga zinazokwenda na utaratibu huo, hasa utofautishaji na ukuzaji wao. Naye Wamitila, K. W (2003:278) anafasili dhana hii kama mbinu za mikakati inayotumiwa na mwandishi kuwasawiri wahusika katika kazi yake. Kutokana na fasili hizi, tunaona kuwa wahusika wapaswa wawe na tofauti za aina aina ambazo zinawatofautisha. Pia wapaswa wakuzwe vizuri.

Syambo na Mazrui (1992:72) wamewafasili wahusika kama wale binadamu wa hadithini ambapo Wamitila K.W. (2003:123) akirejelea mhusika, anasema kuwa huyu ni kiumbe anayepatikana katika kazi ya kifashihi na ambaye anafanana na binadamu kwa kiasi fulani. Wahusika ndio ambao hutenda mambo mengi katika tamthilia na hivyo kuisukuma mbele ploti, bila wao ploti itakwama.

Wahusika huwa wamekuzwa katika viwango tofauti na pia hutekeleza majukumu tofauti na kwa sababu hii, wanaweza kupangwa katika makundi tofauti sawa na ambavyo tunaweza kutofautisha aina mbalimbilili za watu kulingana na tabia na matendo yao katika maisha halisi. Wahusika hupewa sifa za kusadikika na wanajamii kwa sababu matazamio ya hadhira ya kazi ya fashihi ni kumwona mhusika kama binadamu halisi, aliye hai na kama mmoja wao.

Katika fashihi, na hasa tamthilia, mhusika ni kinywa na kiashiria cha msanii. Majukumu yake ni kufafanua na kuwasilisha maudhui, maoni, hisia, mawazo, itikadi pamoja na mtazamo wa mtunzi. Nafasi ya mhusika katika kazi ya fashihi hutegemea uzito ama upevu wa majukumu aliyopewa na msanii. Msanii ana jukumu la kuwasilisha katika kazi yake wahusika

wanaoweza kuaminika wanapotekeleza nyadhifa zao kwa kuwapa sifa na tabia zinazostahili.

Kama tulivyosema hapo mbeleni, tunaona kuwa msuko wa matukio katika tamthilia hutegemea wahusika. Matendo na mahusiano yao ndicho chanzo cha mgogoro ambao hujenga ploti. Vitendo na mazungumzo yao ndivyo ambavyo huchangia katika kuisukuma mbele hadithi na hivyo kuijenga ploti.

3.02 WAHUSIKA KATIKA *WINGU LA KUPITA*

Wahusika wanaopatikana katika tamthilia ya *Wingu La Kupita* wanaweza kuainishwa katika makundi tafouti. Kwa kuzingatia kigezo cha umri, tuna wahusika wa umri wa makamo (Mama na Mwanamke), wazee (Baba na Michonge), vijana (Jaribosi, Kisura na mfungwa) na watoto (Mvulana na Msichana). Zaidi ya uainishaji huu wa ki-umri, tunaweza kuwagawanya wahusika hawa kulingana na majukumu yao, nyadhifa ana nafasi wanazochukuwa katika tamthilia hii. Kulingana na majukumu au nafasi zao tuna wale ambao wamechukuwa nafasi kubwa na wengine ndogo. Hivyo tuna wahusika wakuu na wahusika wasaidizi. Njogu na Chimera (1999:41) wanasema hivi kuhusu wahusika wakuu:

Wahusika wakuu ndio nguzo ya kazi ya kifasihii
na ndio wanaosheheni hadithi nzima. Matendo
na migogoro yote muhimu inawahusu wao.

Kuwahuwu wale wasaidizi, (1999:41) wanasema:

Hawa huwa wanatumiwa ili kumsaidia msomaji
amwelewe vyema mhusika mkuu .

Tofauti za wahusika katika *Wingu La Kupita* zinajitokeza katika hali mbaalimbali na zinadhihirishwa na mahusiona yao, tofauti zao za kiimani na mitazamo yoa kuhusu maisha kwa jumla. Tofauti hizi zinasaidia katika kukuza ploti ya visa vinavyopatikana katika tamthilia hii.

3.03 WAHUSIKA WAKUU

Tamthilia nzima ya *Wingu La Kupita* inahusiana na matatizo yanayoikumba familia moja ya mhusika Baba na Mama. Mambo yote yanayotendeka katika tamthilia hii yanaihuu familia hii kwa njia moja au nyingine. Hivyo, wahusika wakuu wa tamthilia hij ni wale wanaohusiana na familia hii kwa njia ya moja kwa moja. Wahusika ambao wamechukuwa nafasi kubwa ya tamthilia hii ni Mama, Mvulana, Msichana na Baba. Hawa ndio wahusika ambao matendo na mambo mengi juu ya tamthilia hii yanawahuu na wao wanachukuwa sehemu kubwa ya tamthilia hii.

Mama, ambaye ana umri wa makamo, amesawiriwa na mtunzi kama mhusika ambaye hana bahati maishani mwake. Alikuwa ameolewa na mume wa kwanza ambaye pamoja na watoto wake wawili waliuawa na wapora ng'ombe ambao pia walimnajisi kifo hiki cha kilimpelekea kuolewa kwa mara ya pili mume wa sasa (Baba) ambaye hamjali kwa vyovyote na amemwachia mzigo mzito wa kuikimu familia yake. Hata makazi alimoishi ni duni kwani ni banda badala ya nyumba. Kwa hivyo matarajio yake ya kuwa na maisha ya furaha katika ndoa yanakuwa kinyume na hivyo kuleta mshangao kwake.

Licha ya kuwa ana matatizo chungu nzima, mtunzi amemsawiri kama mhusika wa kuigwa na wanawake walio na matatizo kama haya kwa vile alikuwa na bidii katika kuhakikisha kuwa watoto wake walipata chakula, walisoma na alijali mavazi yao. Tunapoichunguza tabia yake kindani tunaona ana utu kwani alimjali mumewe hata ingawa mume huyu hakutulia nyumbani na aliyapuuza majukumu yake. Mama alionyesha utu huu alipomwambia mwanamke kuwa:

Mama: (Anatingishatingisha kichwa kisha anasagasaga na kuanza kuongea kwa sauti ya chini) mtu, unajua tena kama wasemavyo watu, hauvui mji kadamnasi. Kuna mengi lazima umezee japo unabakia kuungulika *ndani kwa ndani*. *Unadhani kuna wangapi unawaona wakicheka Hadharani na nafsi zigo la simanzi lawatafuna kama fuko?* (uk. 18).

Kupitia kwa maongezi haya twaona aliiheshimu familia yake na hakuwa radhi kuaibisha hadharani. Kwani alijua kuwa kulikuwa na wengine waliokuwa na matatizo mengi zaidi ya yake. Tabia hii ndiyo iliyomsaidia kudumisha familia yake. Ametumiwa na mwandishi kama kielelezo cha kuigwa na wanawake wengine waliokuwa na matatizo kama haya katika jamii. Inaonekana alikuwa na tabia ya kupuuza mawaidha ya watu waliyomhusu (mjombaye na Jaribosi) na kufanya uwamuzi wa haraka jambo ambalo lilimpelekea kupata matatizo baadaye na kuishia kujuta. Alionyesha kujuta kwake kwa kusema:

Mama: (Anaonyesha kushangaa baada ya kukiona kile kitii)... kumbe kule kutaharaki kunioa ilikuwa ni kunilazia tu. Kisha nami mpumbavu ... ndio nikamwamini licha ya onyo la mjomba (uk. 9).

Aliendelea kuonyesha kujuta aliposema:

Mama: (Akishusha pumzi)... mie siku zile nikimwona mwanangu kama anayemdharau babake (kwa hadhira) kumbe mwenyewe alijua akisemacho aliposhikilia kuwa kuna kuhadaika na rangi mtu ukasahau chai hutiwa utamu na sukari. Wazazi huenda wakadharau watoto kwa kuwaona wachache wa busara lakini ni kinyume kabisa. (uk. 46).

Tabia hii yake yakupuuza mawaidha ya jamaa zake ndiyo iliyokuwa mwanzo wa taabu zote alizozipata katika ndoa yake ya pili. Kwa hivyo kudharau huku kunachangia katika kuisukuma hadithi mbele kwani kama hangeyadharau na kuyapuuza, tamthilia ingechukuwa

mwelekeo mwengine na mtunzi hangeweza kututolea tahadhari juu ya kuyapuuza mawaidha ya wengine, haswa wanaotuhusu.

Mama alionyesha tabia ya kutowaheshimu walimu mbele za watoto wake aliposema mwalimu alikuwa na kichaa kwa sababu ya kuwaambia watoto baba ni mama. Kitendo hiki kinaoana na hali halisi katika jamii kwani kuna wazazi ambao huwadharau walimu wa watoto wao hadharani. Ingawa hivyo, mtunzi hakuonyesha madhara mabaya ya kitendo hiki kwani hakutuonyesha jinsi watoto hawa walivyoathirwa kimasomo.

Mhusika Baba anaichukuwa nafasi hii ya wahusika wakuu kwa vilié yeye ndiye chanzo cha matatizo yote yanayoikumba familia yake. Anarejelewa wakati mwangi na Mama, watoto na pia Mwanamke. Kupitia kwa maelezo ya Mama mtunzi amemsawiri kama Baba mtu ambaye ni mnafiki kwani alisema :

Mama: Humjui kabisa. Hata mie niliamini vile, asivyopenda kusemasema
nilimdhania hivyo kumbe hata mie sikumwelewa. (uk. 45).

Kupitia kwa matendo yake ya kutoijali familia yake na kutotulia nyumbani tunaona kuwa si mpole kama Mama alivyodhania. Upole wake umo katika kunyamaza tu. Yeye anatumwiwa na mwandishi katika kuwaonya na kuwatahadharisha wanawake wasiwe wakidanganyika na uzuri wa nje wa mtu na hivyo kufanya uwamuzi wa haraka kwani huu ni "Uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti". Mhusika huyu anawakilisha kundi la wale mabwana ambao hawatulii nyumbani na kuzijali familia zao ili ziwaelewe. Baadhi ya madhara ya matendo kama haya ni watoto kuichukuwa nafasi ya baba na kuishia kumsengeňya wakati hayuko. Mama anaieleza hali hii kwa kuisema:

Mama: mwenzangu hatulii nyumbani hata watoto wanaanza kumpiga
vijembe sasa. (uk. 44).

Aliendelea kusema:

Mama: ... labda akitoka (Jaribosi) huku atawatuliza ndugu zake hawa
wanaolalamika kuwa wamekuwa wanachekwa kutokana na baba yao
asiyewajali na kunitua mizigo mie. (uk. 46).

Hapa mtunzi anawaonya wanaume ambao wanatabia kama hii kwani yaliyotendeka kwake Baba yanaweza yakanakende kwa. Ingawa mtunzi alimsawiri mhusika Baba hivi, ameidoofisha plot ya hadithi yake kwani ingekuwa na uhalisia zaidi kama Baba huyu angejitokeza katika tamthilia na kutenda mwenyewe. Hatujui kama yote yanayosemwa juu yake na wale wengine ni ya kweli au la kwani msema pweke hakosi..

Katika kundi hili tuna pia wahusika Mvulana na Msichana. Hawa wanajitokeza mara nyingi katika tamthilia. Ni wao ambao wanaadhiriwa na matendo mabaya ya baba yao moja kwa moja. Wao wana umri mdogo sana kwani katika maelezo ya mtunzi mwanzoni mwa tamthilia, tunaelezwa kuwa Mvulana ana umri wa miaka sita hivi na kwa hivyo nduguye Msichana ana umri wa miaka minane.

Wao ni wanafunzi katika shule ya msingi. Hawana nguo na chakula wanachopewa hakiwatoshi. Ukosefu huu unasababisha wao kuwa ombaomba kwa majirani. Ni watoto wanaopenda kusoma kwani licha ya matatizo haya waliendelea na masomo na walikuwa wakiwatii walimu wao na kuwapenda. Mtunzi amewatumia watoto hawa kutuonyesha jinsi, mfumo wa elimu ambao uliendelezwa katika shule za Peyinatali ulivyokuwa havifai. Mfumo wa zamani wa elimu ulibadilishwa bila mpango na mfumo mpya uliowekwa uliwaleta wazazi hasara kubwa. Mazungumzo kati ya watoto na Mama yao yanadhihirisha jambo hili.

Mama: (Kaachama) kila siku mwabeba vitabu vyta kusoma. Leo ndio mmevi peleka wapi au mmeviacha huko mchangani mnakopita mkicheza kila siku?

Mshichana: (Anadakiza) shule imevichukua; inasema havifai tena mama!

Mama: (Kwa mshangao mkubwa). Havifai tena, ndio tuseme mmeviacha?

Mvulana: Mwalimu anasema kuwa vitaandikwa vingine. (uk. 38-39).

Basi twaona kuwa, wazazi na wanafunzi hawakuwa wamejulishwa mbeleni kuwa kutakuwa na mabadiliko katika mfumo wa elimu. Jambo hili lilifanywa ghafla kupitia kwa watoto twaona jinsi dhuluma zinavyo endelezwa kwa walimu kwa mfano, kuachishwa kazi ovyo ovyo na kupigwa na askari katika nchi hiyo. Twaona basi kuwa, kama watoto hawa wangeondolewa hadithini msomaji hangeweza kuelewa jinsi uhusiano mbaya katì ya baba na mama unavyowaletea watoto hasara na jinsi serikali inavyoweza kuleta hasara kwa kuyatenda mambo ovyo ovyo.

3. 04 WAHUSIKA WADOGO

Kundi hili linawahusika, Jaribosi, Mfungwa, Bosi, Michonge, Sami, Ruksa, Kalimao na Mwanamke. Wahusika hawa wanahuishwa na wahusika wakuu kwa njia moja au nyingine. Mhusika Mwanamke anaonekana kuwa na uhusiano wa karibu sana na Mama kwani wanonekana wakiwa pamoja kwa wakati mwingu.

Mhusika huyu ana umri sawa na Mama na amewahi kuwa na matatizo yanayoshâbihiana na yale ya Mama. Tunaweza kusema kuwa tajriba zao zinazofanana ndizo zinazochangia katika kuwa uhusiano wa karibu. Hii ni sawa na ilivyo katika hali halisi kwani, “waislamu hujuana kwa vilemba”. Ni kupitia kwao ambapo tunaweza kuelewa jinsi kuna matatizo ya kifamilia katika nchi ya Peyinatali. Uhusiano na mazungumzo yao yanaisukuma hadithi mbele kwani kama mwanamke huyu hangekuwepo Mama hangeweza kutujulisha mambo mengi yaliyomhusu. Kwa mfano: jinsi mumewe amemtesa kiasi cha kujuta kuolewa naye, yaliyotokea maishani mwake mpaka akaolewa na Baba na Jaribosi kufungwa.

Kupitia kwa mhusika huyu tunapata kujua kuwa kuna matendo ya kiuchawi yanayofanywa na baadhi ya wanawake ili kuwapumbaza waume zao. Mwanamke alisema:

Mwanake: ... Nikawaona walionitangulia kwa hili wakanipasulia mizungu nami nikaizamia. Mbona nilipoibuka nilimzika janja na hila zake na kumwopoa zumbukuku ulimwengu uko huko.(uk. 18).

Mazungumuzo haya yalifuata yale ambayo mama alitaka kujua ni nini mwanamke huyu alichokuwa amempa mumewe ili atulie nyumbani. Katika kujibu twaona kuwa kuna waliomtangulia Mwanamke huyu katika jambo hilo. Kupitia kuwa kuna imani juu ya uchawi katika jamii hii. Ingawa ni mhusika wa karibu sana na mama, haieleweki jinsi walivyoachana mara ya mwisho walipokuwa pale mtoni wakiteka maji. Ni kama hakuondoka hapo.

Mhusika Jaribosi, ni mwanawe Mama. Ndiye mkubwa wa wale wengine na alikuwa amesoma na kupata kazi katika serikali. Ni mhusika mwenye msimamo dhabiti na aliyewajali raia maskini. Ni kutokana na kuwa na msimamo huu dhabiti uliokuwa tofauti na wa mkubwa wake kazini ambapo alifungwa jela. Kama hangekuwa na msimamo huo na kuwatetea masikini hangefungwa. Kwa hivyo msimamo huu wake unachangia katika kuendeleza hadithi mbele mpaka pale gerezani. Ni kupitia kwake pia ambapo tunapata kuelewa uozo wa viongozi serikalini na dhuluma ambazo serikali inawatendea wanaoipinga katika mipango yake mibaya.

Jaribosi: (Bila kutikisika) Lakini kwa nini bodi imekataa kuzingatia kilio cha watu wanaoishi pale? Watahama waende wapi na hawana pa kwenda wale?

Bosi: (Anaanza kukasirika) umekuwa mbunge wao? ...(uk. 33)

Mwandishi amemtumia kuonyesha kuwa kuna watu wazuri katika jamii ambao wanayajali maslahi ya wengine kiasi cha kuhatarisha maisha yao. Ingawa mtunzi amemsawiri Jaribosi hivi, anamfanya aonekane akiwa wa kukatiza tamaa kwani baada ya kutoka jela hakuendelea na juhudzi zake za kuipigania wanyonge wanaodhulimiwa hata mama yake

amabye anadhulimiwa na mumewe baba. Ingefaa mhusika huyu aendelee na juhudzi zake za ukombozi, haswa pale nyumbani mwao.

Tuna mhusika Mfungwa ambaye alikuwa amefungwa jela moja na Jaribosi. Kabla ya kufungwa kwake alikuwa ameshikilia wadhifa katika serikali ambapo aliendeleza ufisadi. Yeye alifungwa kwa mpango ili serikali iwahandae raia kuwa haiungi mkono kiteendo hicho.

Jaribosi: uliiba nini?

Mfungwa: Pesa za umma. (uk. 25).

Aliendelea kusema:

Mfungwa: Labda hukukosea. (mtuo) kwa kweli sikutakiwa kuwa hapa kabisa: haya ni matokeo ya strategy. Ulikuwa mpango tu kuwa lazima pafungwe mtu ilikuwatiliza makelele yaliyokuwa yakipigwa na kikundi fulani mjini.
(uk 26).

Kupitia kwake tumeweza kujua jinsi maofisa wakuu serikalini huibia raia wake badala ya kuwasaidia. Pengine hali hii ndiyo iliyosababisha umaskini mwangi mionganoni mwa familia katika nchi hiyo na hivyo kuzifanya familia kuvunjika kama vile, ya mwanamke na ya mama ambayo inaelekea kuvunjika kabisa. Mfungwa amechukuwa nafasi ya kutuonyesha, ingawa sio kwa njia ya moja kwa moja, vile matendo mabaya yaweza kuchangia katika kuifuruga jamii kwa kuifanya iwe na umasikini mwangi. Ametumiwa kuendeleza mawazo ya ufisadi katika jamii.

Mshusika mwengine aliye katika kundi hili la wahusika wadogo ni Bosi. Huyu alikuwa mkubwa wake Jaribosi pale kazini. Ni mhusika ambaye hajahitimu vizuri na alikuwa na tamaa sana ya pesa. Tamaa hii ndiyo iliimfanya aibe pesa za umma na kumfanayia fitina ye yeyote aliyempinga katika mipango yake mibaya ya kuibia umma. *Hila zake ndizo* zilizosababisha kufungwa kwa Jaribosi. Alisaidia kuisukuma hadithi mbele kwa

kusababisha kufungwa kwa Jaribosi. Ametumiwa na mtunzi katika kuendeleza mawazo ya ufisadi mionganoni mwa wanaoshikilia vyeo serikalini.

Michonge ni mhusika ambaye hajikotezi katika kazi hii lakini anazungumziwa na wahusika wengine. Yeye ni kiongozi katika nchi jirani na ya Peyanati. Yeye ni tofauti kitabia na Baba ambaye ni kiongozi wa Peyinati. Michonge alitulia nyumbani na hivyo akaweza kuelewa familia yake. Aliweza pia kujali na kuyakimu mahitaji ya familia hiyo.

Msichana: (Kwa manung'uniko) sasa tutakula nini mama, kama unatafuta chakula?

Chakula kinachukua wakati mrefu kabla ya kuiva.

Mama: (Akiwazawaza) kajaribuni huko kwa jirani labda chakula chao kitakuwa tayari.

Msichana: (Anaonyesha wasiwasi) kwa Michonge?

Mama: (Akitikia kwa kichwa) kuko huko, eleee!

Mtunzi amemtumia kuonyehsa jinsi kiongozi mwema anavyopswa kuwa. Tunaona kuwa familia ya baba ilitamani jinsi Michonge alivyoitunza familia yake. Yeye kwa hivyo ni mfano mzuri wa kuigwa.

Ruksa ni mtoto wake Michonge ambaye babaye alikuwa radhi kutwaa uongozi kwake baada ya Michonge kushindwa na uongozi. Ametumiwa na mwandishi ili tuone kuwa kuna viongozi ambao wako tayari kutwaa uongozi kwa wengine lakini sio kama baba ambaye hataki kutwaa uongozi kwa Jaribosi.

Kalimao ni mhusika ambaye pia hajitokezi katika kazi nzima. Yeye alizungumziwa tu na watoto na mama yao. Ingawa hivyo, wao wanatufanya tujue yeye ni mwenye ukarimu na alikuwa na uhusiaono na familia ya baba.

3.05 TATHMINI

kwa kurejelea tamthilia ya Wingu La Kupita, tunaona kuwa kuna wahusika mbalimbali kuna wale ambao wameweza kuichukua nafasi kubwa na wengine ndogo. Wahusika hawa hawakukuzwa kwa viwango sawa. Kuna wale wamekuwa zaidi na wengine kwa kiasi ilhali wengine wanajitokeza katika maongezi ya wengine. Hawa ambao hawajitokezi wanaifanya tamthilia isiwe na mvuto kwani tungetaka kujuu mengi juu yao kwani wengine wao ni wa kupendeza kama vile Michonge. Mshusika Baba ambaye ni chanzo cha matatizo mengi katika tamthilia hajitokezi waziwazi. Kitendo hiki cha kutojitokeza kwake kinaifanya tamthilia isiwe na wapinzani wawili wenye mgogoro ulio na nguvu. Pia hatumwelewi vizuri mshusika Baba. Ingefaa mtunzi amwingize katika tamthilia kwa njia ya wazi ili tamthilia iwe na uhalisia na yenye mvuto kwa msomaji.

Ingwa kuna kasoro hii katika uumbaji wa wahusika, tunaona kuwa mtunzi ameweza kuwatofautisha wahusika wake kwa mfano Baba na Michonge, Jaribosi na Bosi na mfungwa, na Mama na Mwanamke.

3.06 WAHUSIKA KATIKA PANGO

Wahusika katika tamthilia hii wanweza kuanishwa katika njia mbalimbali. Tunaweza kutumia uainishaji wa kijinsia ambao ni wa kijumla mno. Kwa kuzingatia uanishaji huu tuna wahusika wanaume kama vile; Ngwese, Seki, Babu, Kibwana, Kauleni, Ngoi na Kikubi. Tuna wale ambao ni wanawake. Kwa mfano; Katango, Mama, Susa na Sota. Wahusika wanaume wemeichukua nafasi kubwa katika tamthilia hii. Kwa kuzingatia umri, tuna wahusika wazee, wa umri wa makamu, na watoto. Wahusika wazee ni; Ngoi, Babu na Malebo. Wahusika wa umri wa makamu ni: Ngwese, Seki, Sakina na Mama. Wale ambao ni vijana ni wengi. Hapa tuna: Katango, Kikubi, Kauleni Mbambekazi na Kibwana. Kundilala watoto lina: Susa na Sota.

Kwa kuzingatia nafasi zao katika tamthilia, tuna wahusika wakuu na wale wadogo. Wahusika wakuu ni Ngwese, Katango, Susa na Sota na wadogo ni kama vile: Seki, Mama, Babu na Ngori.

3.07: WAHUSIKA WAKUU

Mbunda, M. (1993: 33) amewafasiri wahusika hawa kuwa ni wale ambao wanajitokeza kila mara katika kazi za fasihi tangu mwanzo hadi mwisho. Wahusika hawa ni wale ambao tayari tumewataja. Mhusika Ngwese niwa umri wa makamo, ni tajiri kwani ana shamba na nyumba maridadi na ametoka katika nasaba ya uongozi. Anasema:

Ngwese: ... Najua kuwa uongozi ni jadi yetu, umechanjiwa kwenye ukoo na
nasaba yangu tangu zama za mababu. (uk. 8).

Anaendelea kusema:

Ngwese: ... nani mwingine isipokuwa mimi ambaye nimekulia katika
nyumba ya utawala? (uk. 11).

Kuwa alikuwa amekulia katika nyumba na ukoo wa uongozi ndiposa alitaka kuwa kiongozi wa Pang'o. Jitahada hizi zake za kutaka kuwa kiongozi zilimfanya kutangaza kuwa angewania kiti cha uongozi. Azma hii ndiyo iliyompelekea kufanya kila juhudhi za kuutwaa uongozi huo. Lolote alilolifanya lilekezwa katika harakati zake za kutwaa uongozi. Kwa hivyo azma hiyo inasaidia katika kuisukuma hadithi mbele kwani uongozi hauchukuliwi hivi hivi, ni lazima mgombezi wa uongozi akabiliane na wengine ili auyakue.

Kwa vile alitaka uongozi, aliweza kukabiliana na mpinzani wake wa pekee- Katango kwa kila njia. Matendo aliyoyafanya katika harakati hizi yalikuwa mengi. Kwa mfano: Kumshambulia Katango, kuwakataza watoto kuteka maji na kadhalika. Hana huruma. Tabia hii ya kukosa huruma ndiyo iliyompelekea kuwakataza na kuwafukuza watoto Susa na Sota walipokuwa wakienda kisimani kuteka maji. Makelele aliyowafanyia wale watoto

yalisababisha bibiye Sakina kufika mahali hapo na kutaka kujuua sababu ya ugomvi. Mgogoro unazuka baina yao na mtunzi akausuluhisha kwa kumwondo Sakina na Ngwese akabaki akijizungumzia. Kwa hivyo tunaona jinsi tabia ya kinyama inavyosaidia kuisukuma hadithi mbele.

Tabia yake ya kuwa na taasubi ya kiume, ilimfanya kuwadharau wanawake sana. Ndiyo iliyomfanya kumtukana Katango, walipokutana. Anamwambia Katango:

Ngwese: (Akijisemea) Ahh. Kisirani chenyewe hiki hasa! Babu alisema kukubana na mwanamke asubuhi ni kisirani, siku nzima anaichafua. (kwa Katango)
Mwanamke, unasaka nini hapa"? (uk. 10).

Maneno haya ndiyo yalioanzisha mgogoro baina yao ambapo Ngwese aliendelea na kuonyesha madharau kwa wanawake, haswa Katango, naye Katango akijitetea na hapo hapo kila mmoja akamjulisha mwingine azma yake ya kuwa kiongozi. Kama Ngwese hangekuwa hivyo, mtunzi hangeweza kutondokezea lengo la kila mmjoja mapema hivyo.

Ni mwenye ujisadi kwa vile aliwahonga watu wakati wa uchaguzi na sababu hiyo ikamfanya achaguliwe. Ni ujisadi huo uliomfanya afungwe baada ya kuchaguliwa na hivyo kumwachia Katango uongozi.

Mhusika mkuu mwingine ni Katango. Ni mhusika mwanamke ambaye ni kijana. Amesoma na kuwa mwalimu. Huyu ni mpinzani wake Ngwese katika kutaka kupata uongozi wa Pango. Ni msichana ambaye ni jasiri kutoka utotoni alipokuwa mwanafunzi shulenii (uk..25), Kikubi anasema hivi kumhusu Katango:

Kikubi: Ahh huyo? (mtuo)nimesoma naye..aliwahenyesha
wanaume ile mbaya kutokana na misimamo
yake. Ana ujasiri sana.

Twaona hata nyumbani kwao ana ujasiri kwani anapingana na baba^{ke} (Seki) katika mambo mengi K.m kutenda kinyume cha utamaduni na kukataa kufanyiwa tohara. Anakabiliana na Ngwese wakati Ngwese aliwafukuza ndugu zake, yaani: Susa na Sota walipokuwa wakienda kisimani (uk. 10).

Ingawa ni kijana asiye na pesa kama Ngwese amejitolea kumpinga katika uongozi wa Pango na anajitolea hata kupigwa na kutukanwa katika harakati zake za kuwanja uongozi huo ingawa yeye ni mwanamke na katika jamii yake mwanamke hatarijiwi kuania uongozi. Ingawa amesawiriwa hivi hatujui kiwango kipi cha shule anapofundisha, shule za msingi, sekondari au vyuo. Elimu aliyonayo ndiyo iliyomfanya awezé kujifahamu zaidi na kufahamu matatizo yaliyoikumba jamii yake na hivyo akaamua. kupigania uongozi wa Pango.

Hana ubinafsi. Katika (uk. 9) alikilaumu kitendo hiki cha ubinafsi katika mjadala nafsi,. Anasema hivi:

Katango: “Ehh mara hii asali ya pangoni lazima iwafaidi wote..” (uk. 28).

Msimamo wake wakuwajali wengine ndiyo uliomumotisha katika kupagania uongozi wa Pango ili kuwaondoa wale ambao wamejawa na ubinafsi kama Ngwese.

Yeye ni kiwakilishi cha kizazi kipyä ambacho kinapinga utamaduni unaoendeleza dhuluma dhidi ya wanawake. Utetezi huu ndiyo unaochangia katika harakati zake za kugombania uongozi ili awakomboe waliodhulumiwa. Kwa hivyo tabia hii yake inachagia katika kuisukuma hadithi mbele. Mwanzoni alishindwa kuchukuwa uongozi na Ngwese lakini kisadifa Ngwese alichukuliwa na polisi na kumwachia Katango uongozi. Ni mhusika wa kuigwa katika jamii ya kisasa.

Wahusika wengine ambao ni wahusika wakuu ni Susa na Sota .Wahusika hawa tunawachukulia kuwa katika kundi hili kutokana na ufanuzi wa Mbunda Msokile kuwa wao hujitokeza mara nyingi katika tamthilia. Hawa wawili ni ndugu wadogo wa Katango.

Sota ni mvulana wa miaka kumi na mmoja na susa ni msichana wā miaka kumi. Wahusika hawa humsaidia mama yao kazi za nyumbani, kama vile: kuteka maji. Ni watoto walio na ujasiri mwingi kwa mfano, walipoambiwa na Ngwese wasiende kuteka maji, kisimani, walismama na kujitetea badala ya kutoroka hata ingawa Ngwese akiwa mwenye hasira nyingi kwao. Walikabiliana na wale watu waliompiga Katango na Kibwana pale barabarani (uk. 33). Pia hawakuogopa kwenda kisimani hata baada ya baba yao kuwaambia kuwa pangoni pana subiani (uk. 22) na hata walipoenda pangoni kuona kama kwamba nyuki wamerudi (uk. 64) na wakasikia sauti ya kutisha hawakukimbia kuondoka bāli walikaa hapo na kuchungulia mpaka wakamwona Katango ambaye ndiye alikuwa pale.

Pia walipoisikia sauti nyingine (Uk. 79) hawakutoroka. Kulingana na ujasiri huu wao, mtunzi ameweza kuiendeleza hadithi mbele kwa vile ni kupitia kwao tunapata kujua kuwa Ngwese hana huruma hata kwa watoto. Tunapata kujua yale yanayoendelea pangoni. Ingawa mtunzi amewasawiri hivi, kuna sifa hii ya ujasiri wao ambayo ameitia chumvi kwa vile katika hali halisi ni nadra kuwapata watoto wadogo kama hawa wakiwa na ujasiri wa kiwango hicho cha kutembelea mahali kama pango ambapo waliambiwa kuna subiani na babu yao. Pia alikuwa amewajulisha kuwa mashetani huishi mle pangoni. (uk. 63) kwa hivyo hatungetaraja wakae pale pangoni walipoisikia ile sauti ya ajabu kwani wangeichukulia kuwa ya wale mashetani walioambiwa juu yao na babu yao.

Jambo hili linatufanya kuwaona kama wahusika ambao sio wa kuaminika kwani, katika hali halisi watoto kama hawa huwa na uoga mwingi na hivyo hawangeweza kupatembelea mahali kama pale penye hatari hizo.

3.08 WAHUSIKA WASAIDIZI

Ingawa wahusika hawa ni wengi katika tamthilia ya *Pango* tunaona kuwa kuna wāle ambao wamechukua nafasi kubwa kuliko wengine. Wahusika hawa ni kama: Sakina, Mama, Seki, kijana Kauleni, Mbabekazi, Kikubi, Kibwana, Ngoi, Babu, Mtū I, Mtū II, Jitu I, Jitu II, Polisi I, Polisi II.

Seki ni babake Katango, Susa na Sota. Ni baba ambaye amesawiriwa na mtunzi kama asiyeipenda familia yake kwani anaungana na Ngwese katika kumhangasha bintiye (Katango) ambaye anampinga Ngwese. Tungetarajia Seki amuunge mkojo bintiye Katango katika harakati za kuwania uongozi wa Pango lakini Seki anafanya kinyume cha matarajio hayo na hivyo kumfanya msomaji aachwe akishangaa juu ya tabia hii ya Seki.

Twaona pia kuwa anasingizia watoto wake Susa na Sota kuwa ndio wachezao kisimani ilhali ye ye akijua vizuri kuwa sio wao lakini ni akina Ngwese wachezao mle kisimani. Anashikilia utamaduni sana. Kwa mfano, alitaka bintiye Katango afanyiwe tohara na pia anamkemea wakati alipoenda nyumbani akiwa na uta na mishale . kitendo hiki kinaibua mgogoro baina ya Katango na Seki na kusababisha tataruki kwa msomaji ya kutaka kujuu kitakacho tokea baina yao.

Kuna ukinzano wa kimawazo kwani Seki anapinga baadhi ya mambo sababu ikiwa kuwa hayafai katika utamaduni wao lakini mengine anayoyafanya yanapingana na utamaduni huo huo. Kwa mfano; kumwelimisha Katango ambaye ni msichana. Ni mwenye vitisho bila vitendo kwani hata baada ya kumkemea Katango kwa kuwa na uta na mishale, hakuna lolote alilomfanya Katango na tungetarajia amwamrishe aitupe mishale na uta. Pia alikuwa na uwezo wa kumfanya Katango afanyiwe tohara lakini katika (uk.19) anakili kuwa Katango aliligomea jambo hilo na Seki akamruhusu kwendelea kukaa kwake na hata kumuelimisha. Mambo haya yanamfanya aonekane kama baba ambaye hana utawala katika familia yake.Ni mhusika anayesaidia kuisukuma hadithi mbele kwa vile anakuwa kikwazo kwa Katango naye Katango anajibidisha kukiweza kikwazo hicho.

Sakina ni mhusika mwengine ambaye ni wa kundi hili. Ni mkewe Ngwese. Arijitokeza mara mbili tu katika tamthilia mwanzoni baada ya Ngwese kuwafukuza watoto na mwishoni baada ya Ngwese kuchaguliwa kuwa kiongozi kwa hivyo hatuyajui mengi kumhusu. Ni bibi mwenye ujasiri na ambaye ana utu. Tabia hii ndiyo iliyochangia katika kuwatetea wale watoto wawili na pia mwishoni kumkumbusha mumewe wajibu wake wa

kuhudhuria kazini. Tabia hii ndiyo inasababisha mgogoro baina yake na mumewe na hivyo kusaidia katika kuisukuma hadithi mbele.

Mhusika Mama ni mkewe Seki. Ni mama anayeipenda familia yake na anajiali. Anamwunga mkono Katango katika harakati zake za kupigania uongozi kinyume na mumewe Seki. Ni mpole. Tabia hizi hazichangii sana katika kuiendeleza hadithi mbele.

Mhusika Ngoi ni mhusika ambaye anajitokeza kwa mara chache katika tamthilia. Hatujui mambo mengi yake kwa vile anachukua nafasi ndogo mno. Ingawa hivyo, twaona kuwa yeche ni mfuasi sugu wa Ngwese. Anamuunga mkono katika kuwania uongozi wa Pango. Pia yeche anashikilia utamaduni. Twaona kuwa ana mawazo tofauti na yale ya mumewe juu ya mambo mbalimbali kwa hivyo kuna ukinzano wa kimawazo kati yake na mumewe. Ukinzano huu unasaidia katika kuendeleza hadithi mbele.

Vijana Kibwana na Kikubi ni marafiki zake Katango. Wao wanamfahamu Kataango vizuri kwa vile walipata kusoma naye na ni vijana ambao wako tayari kumuunga mkono. Kibwana ndiye mfuasi sugu wa Katango. Ni kutokana na hali hii ambapo anajitolea kumtetea Katango kwa njia zozote. Uwamuzi huu wa kumuunga mkono Katango unamfanya aingie katika migogoro na hata vita na watu wengine. Hali hii inachangia katika kuijenga na kuiendeleza hadithi. Kikubi ni mwénye wasiwasi katika kushinda kwa Katango kwa vile anaona utamaduni utakuwa kikwazo kwani watu wengine katika jamii hii wana taasubi ya kiume. Kundi hili la vijana linapingana na lile la wazee katika mambo ya utamaduni. Kupingana huku kunazuwa mgogoro baina ya makundi haya mawili. Mgogoro huo unasaidia sana katika kuijenga ploti na kuisukuma hadithi mbele.

Mtu I na Mtu II ni wale ambao wanatumiwa na Ngwese katika kumhangisha Katango hata kwa kumpiga. Hawa ni vibaraka vyake Ngwese. Wao wanajitokeza pale hotelini tu na njiani wanapompiga Katango na Kibwana. Ni kuitia kwao ambapo tunaelewa jinsi Ngwese alivyo na tamaa ya uongozi. Kwani anawalipa ili wampinge na kumhangisha mpinzani wake.

Jitu la kwanza na la pili ni wahusika ambao mtunzi amewaita hivi kwa vile vitendo vyao kama inavyodhihirika mwishoni mwa tamthilia ni vya majitu wasiowajali wengine. Hawa majitu ni Ngwese na Seki kama inavyo dhihirika baada ya Katango kuwafunua mwishoni mwa tamthilia. Ni kuitia kwao ambapo mtunzi anadhihirisha kwa msomaji ukweli kuwa Ngwese na Seki na wengine kama Ngori ndio wanaotenda mabaya yote pale pangoni.

Wahusika polisi I na wa II wameingia tu pale mwishoni mwa tamthilia kumshika Ngwese kutokana na kosa la kuvuja mali ya umma. Walitekeleza wajibu wao wa kumshika na baada ya kumshika wakaenda naye na hivyo kutwaa nafasi ya uongozi wa Pango kwake Katango. Mtunzi amewaiingiza polisi hawa katika tamthilia ili tamthilia hiyo ikamilike kwa jinsi ambavyo Katango atakuwa kiongozi. Ni kama kwamba alikuwa ameamua kutoka mwanzoni kuwa Katango ndiye atakayeichukua nafasi hiyo. Ijapokuwa uongozi huo unatolewa kwa Katango kwa njia isiyo na uhalisia.

3.09 TATHMINI

Baada ya kuisoma tamthilia ya *Pango*, tunaweza kuwatofautisha vizuri wahusika wakuu wawili Katango na Ngwese ambao ni wapinzani katika tamthilia. Pia ameweza kuonyesha makundi mawili ambayo yana msimamo tofauti. Kama vile kundi la wazee wanaume lilnaloshikilia utamaduni na kuona kuwa uongozi wapaswa uwe wa wanaume tu. Tuna lile la vijana ambalo lina msimamo tofauti na lile la wanaume wazee.

Ingawa hivyo, kuna wahusika ambao mtunzi amewaingiza bila sababu yoyote inayo husiana na matukio ya hadithini. Kwa mfano, wale polisi wawili ambao wanaletwa na Mbabekazi mwishoni mwa tamthilia ili wamshike Ngwese. Tunaachwa tukijiuliza swali la kwani Mbabekazi ni nani? Aliweza kujua vipi kuwa Ngwese ni mhalifu wa kufuja mali ya umma? ama ni yeze aliyewaita wale polisi waje wamshike Ngwese au ilitokea tu kisadfa wote watatu wakawa pamoja.

Pengine mtunzi angeweza kuifanya tamthilia hii ijumuushe mambo mengi ili wahusika wengine waweze kukubalika katika akili za msomaji lakini sio wanavyoonekana kama wahusika wa kiajabuajabu ambao wanaingia na kotoweka bila kueleweka vizuri.

SURA YA NNE

4.0

MATUMIZI YA LUGHA

4.01

UTANGULIZI

Lugha ni chombo muhimu cha mawasiliano ambacho hutumiwa na wasanii katika kuunganisha vipengele mbalimbali vinavyoijenga fani katika kazi yoyote ya kisanaa. Msanii huwa ana wazo analotaka kuliwasilisha kwa hadhira yake. Wazo hili ataliwasilisha kupitia lugha. Msanii huyo huteua miundo ya lugha inayoweza kuwasilisha na kufanikisha mawazo yaliyo katika kazi yake.

Uteuzi wa lugha wa msanii hutegemea mambo mbalimbali. Syambo na Mazrui (1992:100) wamesema kuwa:

Lugha inaweza kutegemea hali kama vile hasira, furaha, utanzu, sajili, mukthadha, tabaka n.k Wanaendelea kusema kuwa lugha inahitaji kuwatofautisha wahusika kulingana na jinsia yao au umri wao .

Lugha anayotumia mwandishi ni lazima iweze kuwa na sura za usanii na ujumi na pia iweze kuwasilisha mada inayotazamiwa

Ngara, E (1982:10) katika kuonyesha umuhimu wa lugha anasema:

Ingawa kazi ya kisanaa huwa na vipengele mbali mbali k.v
ploti, maudhui na wahusika bila lugha vipengele hivi havitakuwa
na maana.Lugha ndicho kigezo cha kupimia kufaulu au kushindwa kwa msanii.

Kuna uhusiano wa karibu sana baina ya fasihi na lugha. Wellek na Warren (1949:174) wameueleza uhusiano huu hivi:

Lugha ndicho chombo kinachotumiwa na watunzi
Wa kisanii. Kazi ya kisanaa
huundwa kutokana na uteuzi wa
miundo maalum ya lugha fulani.

Senkoro (1982:13) anasema kuna aina mbalimbali za matumizi ya lugha . Aina hizi ni kama vile; tamathali, lahaja nafsia za wahusika , uchaguzi wa msamati, miundo ya sentensi, ufundi wa kutoa maelezo ya wahusika, maelezo ya mandhari na utamu wa lugha itumiwayo.

Kama tulivyosema hapo mbeleni, lugha hutumiwa kuambatana na utanzu ambao msanii anautungia. Anaweza kutumia lugha ya maelezo, majibizano, kishairi na nathari, ingawa wakati mwingine unaweza kupata miundo ya lugha ya utanzu fulani katika utanzu mwingine, kwa mfano : lugha ya kishairi kupatikana katika utanzu wa tamthilia. Kuhusu lugha ya tamthilia , Syambo na Mazrui (1992:99) wanasema kuwa:

Lugha ya mazungumzo inayotumika katika utanzu wa tamthilia
ni muhimu iwe na uwezo wa kuzua na kuendeleza matendo
ya wahusika wake. Mazungumzo ya wahusika ndiyo yanayotupeleka
mbele katika ploti .

Kwa hivyo twaona kuwa, tamthilia husukumwa mbele na majibizano ya moja kwa moja baina ya wahusika walio katika tamthilia hiyo. Lugha hii huwa na sura za lugha hai itumiwayo na wanadamu halisi . Kaida hii hufuata sifa za sura za wahusika. Tamthilia ndiyo utanzu ambao hutazamiwa kudhihirisha mawasiliano kama yanavyopatikana katika majadiliano na majibizano katika hali halisi.

Matumizi ya lugha hutazamiwa kuoana na miktatha ya mazingira mbalimbali inamotumiwa kama wasemavyo Syambo na Mazrui (1992:99) kuwa ;

Muktadha wa lugha huathiri maana ya neno, sentensi au sehemu fulani ya kazi ya fasihi . Kwa hivyo lugha itumiwayo katika utanzu kama vile tamthillia huashiria uteule ili maana anayokusudia msanii ipatikane katika muktadha ule.

Msanii huteua lugha atakayotumia katika kazi yake ili iweze kuleta mguso anaotaka, ujumi au ufasaha wa kisanaa na hivyo aweze kufanikisha uwasilishaji wa mawazo yake kwa hadhira yake. Katika jamii halisi tunapata kuwa, watu mbalimbali hutumia lugha ile ile kwa namna tofauti k.m wazee hutumia lugha iliyo na msamiati, tamathali za usemi na mafumbo ambayo hayaeleweki kwa urahisi na vijana . Mara nyingi Lugha yao huwa na ukale na ambayo imekomaa .

Lugha ya wanawake huwa tofauti na ya wanaume ingawa wote wanaweza kuwa ni wa umri sawa . Lugha ya vijana huwa imeathiriwa na mabadiliko aina aina ya kimuundo na kimsamiati. Wao

hutumia lugha yenye usasa mwingi. Vijana hao huwa wamezua aina yao ya lugha ambayo huwa ni wao tu wanaoielewa na kuifahamu na hivyo huwa inakatiza na kutatiza mawasiliano baina yao na wazee. Mara nyingi huwa ya kuendeleza siri zao. Wakati mwagine wao huchanganya ndimi.

Matumizi ya lugha yanayofaa muktadha na malengo ya msanii hufanikisha mawasiliano kati ya fanani na msemaji. kama asemavyo Ngara (1982:10) kuwa :

Uamilifu wa lugha ni kuleta mawasiliano . Ili kuleta mawasiliano yafaayo ni lazima msemaji (mtunzi) atumie lugha kwa njia inayoleweka na msikilizaji au msomaji.

Mtunzi anapaswa kutumia lugha ya kisanaa ambayo ina uwezo wa kuteka makini na kumwathiri msomaji wa kazi yake. Lugha isiyo na usanii na ujumi huweza kumchosha na kumkatisha hamu msomaji. Lugha ya Sanaa yapaswa ivutie ili iweze kunata mawazoni bila hisi za msomaji na iweze kujenga picha mawazoni kwani kama asemavyo Ngara (1982:10):

Lugha ndicho kigezo cha kupimia kufaulu au kufeli kwa mtunzi.

4.02

LUGHA KATIKA WINGULA KUPITA

Kwa vile lugha ni chombo cha mawasiliano yapaswa iendeleze mawasiliano katika maongezi yoyote lakini sio iyatatize. Kama ilivyo katika hali halisi, lugha yapaswa irahisishe mawasiliano, vivyo hivyo yapaswa itekeleze jukumu hilo katika kazi za kisanaa. Utata wowote ukitokea katika matumizi ya lugha, kutakuwa na ukosefu wa mawasiliano baina ya wanaohusika katika mazungumzo hayo. Katika jamii yoyote huwa tuna makundi mbalimbali ya watu ambao huwasiliana kwa njia moja au nyingine. Tunaweza kuwa na wazee wakiwasiliana mionganoni mwao, wakiwasiliana na vijana, na wazee na vijana wakiwasiliana mionganoni mwao.

Huwa kuna jinsi lugha hutumiwa wakati wa mawasiliano baina ya makundi haya katika jamii na hali hii yapaswa kuwakilishwa katika kazi ya fasihi yoyote ile haswa tamthilia. Tunatarajia wazee wawe na lugha pevu yenye msamiati mwingi, methali, nahau, n.k ilhali ile ya vijana iwe yenye

ukavu na wakati mwingine iwe yenyе mseto. Katika tamthilia ya *Wingu La Kupita*, kama ilivyo katika hali halisi ya maisha, mtunzi ameyasawiri makundi mbalimbali ya wahusika. Kwa kuzingatia ujumla wa maisha, tuna wahusika wanaume na wanawake. Pia tuna wahusika vijana, watoto na wazee kama ilivyo katika hali halisi ya maisha. Kwa hivyo tunaona kuwa mtunzi amejaribu iwezekanavyo kuakisi hali halisi ya makundi ya watu wanaopatikana katika jamii.

4.03

LUGHA YA VIJANA

Katika tamthilia hii ya *Wingu La Kupita* kuna makundi mawili ya vijana. Kuna wale walio na umri mdogo sana ambao wamo katika shule ya msingi na ambao hawajapewa majina halisi lakini wanatambulishwa kama mvulana na msichana. Kuna vijana ambao wamefikisha umri wa kuoingawa hawajaoa . Hapa tuna : Jaribosi na Bosi na tuna wale wenye umri mdogo kuliko hawa wawili k.m Kisura ambaye ni katibu wa Bosi. Kati ya makundi hayo ya vijana, kundi ambalo linachukua nafasi kubwa katika tamthilia ni lile la vijana wenye umri mdogo yaani msichana na nduguye mvulana. Katika hali ya kawaida, tunatazamia lugha ya vijana wadogo wa shule za msingi kuwa isiyokomaa kama ile ya watu wazima. Kwa hivyo matumizi ya lugha yao ni holela. Tunatarajia iwe imelegezwa ama ipuuze baadhi ya kanuni za lugha.

Wakati mwingine yaweza kuwa isiyo na utaratibu ufaao haswa inapokuwa siyo lugha yao ya kwanza. Lugha ya vijana hawa wadogo huwa imekosa msamiati pevu na hivyo ni kavu na wao huwa hawaelewi msamiati mwingi unaotumiwa na wakubwa wao. Katika tamthilia tunaona mhusika Mvulana akitaka kujua maana ya neno “*kichaa*” lililotumiwa na mamake. Neno hili lilitumiwa na mama baada ya msichana kusema kuwa walikuwa wameambiwa na mwalimu wao kuwa baba na mama ni sawa. Mama alichangazwa na dai hilo na hivyo alisema:

Mama: Ahh msiyafuate ya mwalimu wenu huyo, ana kichaa.(uk. 2)

Na hapo mvulana aliuliza:

Mvulana: (Anaonyesha dukuduku kubwa)Mama, kichaa ni nini? (uk.2)

Katika kuuliza maana ya neno (*kichaa*) tunaona kuwa mtoto huyu ana upunguvu wa msamiai kwani neno kichaa sio neno gumu kwa yule ambaye amealelewa katika lugha ya Kiswahili. Katika mazungumzo yanayoendelea hapo mbele, tunaona kuwa mhusika huyu mvulana hajui kuwa neno ndovu na neno tembo yana maanisha kitu kimoja . Alisema :

Mvulana: Hapana. Sio ndovu aliiwa tembo. (uk. 4)

Mtunzi ameweza kuwapa watoto hawa, mvulana na msichana lugha inayooana vizuri na umri wao. Baada ya kuambiwa paukwa na mama yao, wote wawili wanajibu :

Mvulana na Msichana: Pakaawaaa! (uk. 5).

Tunaona wao wamerefusha sauti /a/ katikati mwa neno na pia mwishoni. Neno lenyewe lapaswa kutamkwa *pakawa*.

Hii ni hali halisi tunayoisikia ikitumiwa na watoto wa umri huu haswa shuleni wakati wa hadithi. Pia wamerefusha sauti /e/ katika *ehe* wakiitamka *ehee*. Twaona wanaitumia hali hii ya kurefusha sauti kama hali ya kuhamasisha mama yao ili aendelee na hadithi kwa vile wanamsikiliza na wanaifurahia. Wakati mwengine wanaitumia hali hii kwa kusositiza na kubembeleza ili matakwa yao yatimizwe. Walipokuwa shuleni na kuwa na njaa nyingi, kila mmoja wao alisema:

Msichana: Mama nasikia njaa kalii!

Naye Mvulana alisema hivi :

Mvulana:

Mama nina njaa kalii. (uk. 10).

Huu ni ukiushi wa lugha katika kiwango cha kifonolija ambao unafunywa na watoto wa umri huu kwa kusudi ambalo tayari tumelitaja hapo mbeleni.

Kundi lile jingine la vijana ni wale ambao wana umri mkubwa ambao wamemaliza masomo yao ya shule za upili na kuweza kujipatia kazi mbalimbali. Hawa ni: Jaribosi, Mfungwa na Kisura. Katika hali ya kawaida, tunatarajia vijana kama hawa ambao wamesoma hadi kuwa na shahada kama Jaribosi alivyo, wawe na mazoea ya kuchanganya ndimi haswa Kiswahili na Kiingereza. Jambo hili la kuchanganya ndimi linatazamiwa katika jamii ya kisasa. Vijana ambao wamesoma na kuzifahamu lugha zaidi ya moja haswa katika nchi za Kiafrika ambazo hazina sera madhubuti juu ya matumizi ya lugha huchanganya lugha mbili au zaidi haswa lugha ya Kiafrika na ya Kigeni ambayo ni ya wakoloni waliowatawala. Wao huiona lugha ya wakoloni kama yenze hadhi na hivyo kuwa ya wasomi. Wao huitumia ili waonekane wameelimika na ni wa tabaka la juu kielimu. Jambo linalowafanya vijana hawa watumie lugha ya mseto ni mabadiliko ya maendeleo na ustaarabu.

Lugha za kigeni kama vile Kiingereza zinachukuliwa kama lugha za kuonyesha kuwa mtu ni msomi na hivyo ni lugha yenze hadhi ya juu. Vijana waliosoma basi huitumia hapa na pale kuonyesha kuwa wao wamestaarabika kama wazungu wenyewe lugha hiyo.

Ingawa mbinu hii ya kuchanganya ndimi mionganini mwa vijana wasomi inachukuliwa kama njia ya kuashiria hadhi ya juu, inaweza pia kuashiria udhaifu wa kutomakinika katika lugha wanayoitumia; yaani kutokielewa Kiswahili kikamilifu.

Tabia hii ya kuchota na kutumia maneno kutoka lugha mbalimbali hurahisisha mawasiliano haswa kwa mtu ambaye hajazimudu lugha hizi zote barabara. Uhamishaji wa ndimi huifanya lugha ya vijana hawa wasomi ikose mtiririko wa kisarufi. Katika tamthilia ya *Wingu La Kupita* mhusika Jaribosi anaonyesha hali hii ya kuchanganya ndimi. Katika mazungumzo kati yake na mfungwa, Jaribosi alizungumza jinsi hii:

Jaribosi: (Akifurahi) kumbe tuna mawazo sawa ndugu, wanasema
“birds of the same feathers flock together ?”

Aliendelea kuchanganya ndimi katika mazungumzo yake:

Jaribosi: (Anachekacheka) labda ni “class struggle”.

Katika (uk. 34 na 35) alitumia Kiingereza, “progressive” (uk.34), “team” (uk 35), “Imprest”, (uk. 35) na “amorphous absolute”. Mhusika Mfungwa pia alitumia hali hii ya kuchanganya ndimi katika maongezi yake. Ingawa hivyo tunaona kuwa yeze hana umahiri wa kutumia lugha hii. Badala ya matumizi yake kumfanya aonekane mwenye elimu na hivyo mwenye hadhi, yanamfanya aonekane asiye na elimu ya kutosha ingawa amepewa kazi yenye mamlaka makubwa. Hivyo msomaji anaachwa akitilia shaka uwezo wa Bosi huyu kuweza kutekeleza wajibu wa kazi yake ipasavyo.

Mifano ya kuchanganya ndimi kwa mhusika huyu ni kama aliposema:

Mfungwa: ... haya ni matokeo ya “strategy” (uk.. 26)

Aliendelea kutumia maneno “turbines” (uk 28) “weather forecast” (uk. 28), “you have hit the head on the nail” (uk. 29) “mall”(uk.29) na “class struggle” (uk. 30).Tunaona hana umahiri wa lugha ya Kiingereza kwa sababu katika Kiingereza sanifu tunasema: 'You have hit the nail on the head' lakini si kama alivyosema.

Twaona kuwa kwa jumla lugha ya vijana waliokomaa kiumri na kielimu wana kiwango cha hali ya juu cha usanifu na ufasaha wa lugha. Wameweza pia kutumia lugha ya mseto.Mtunzi ameonyesha tofauti za kielemu baina ya Jaribosi na Mfungwa kwa kuwapa umahiri tofauti wa lugha ya Kiingereza kwani kuwa na matumizi mazuri ya Kiingereza inaashiria hali ya kuwa mtu amehitimiz vizuri kielimu

LUGHA YA WAZEE WA MAKAMO.

Wahusika ambao wamo katika kundi hili ni mamake Jaribosi, mwanamke na Bosi. Wote hawa ni wahusika ambao ingawa ni wazee sio wazee sana. Lugha ya wazee hutazamiwa kuwa na utajiri mwingi wa amali za kijadi kama vile mafumbo, misemo, msamiati mzito, methali, nahau na tamathali mbalimbali zinazoirembesha na kuipa lugha uzito wa maana na matumizi. Lugha yao inatazamiwa pia iwe na hekima na busara.

Ingawa lugha ya watu hawa inatazamiwa kuwa yenye heshima haswa inapotumiwa mbele ya watu wa rika la chini ili wale wadogo waige maadili mema na heshima kutoka kwa wakubwa wao, kuna wakati ambapo hawa wazee wanatumia lugha isiyo na heshima wala hekima.

Mfano mzuri ni pale ambapo mhusika mama aliposema mwalimu ana "*kichaa*".

Alikuwa amesema :

Mama: (Akionyesha kukanganywa na maneno ya msichana)

Ahh msiyafuate ya mwalimu wenu huyo, ana kichaakama si wazimu
huo ni nini basi? (uk. 2).

Tungetarajia mama, ambaye ndiye mfano wa kuigwa na watoto wake, atumie lugha yenye heshima haswa tunapozingatia kuwa watoto hawa ni wanafunzi wa mwalimu yule. Kwa kusema hivi, huyo mama anawafanya watoto wale wamkosee heshima mwalimu wao na hivyo wasiweze kufuata maagizo watakayopewa na huyo mwalimu kwani wataona kuwa yeye ni mwendawazimu kama mama yao alivyosema pale nyumbani. Mama yuyu huyu aliendela kutumia lugha chafu isiyo na heshima. Alimduisha mtoto wake na kuonyesha dhara alipotumia neno "*kitoto*" katika kumrejelea mwanawe. Twaona kuwa alitumia lugha yenye dhara nyingi alipouliza swali lenye kejeli sana. Aliuliza:

Mama: unahu nini wimbo wa mwalimu wenu? (uk. 3).

Ingawa kuna chembe ya ukosefu wa heshima katika lugha ya mhusika huyu, alitumia misamiati kadhaa katika maongezi yake. Jambo hili linaonyesha kukomaa kwake kilugha. Kwa mfano:

kusukutua (uk. 7), kutaharuki (uk. 9), kunilazia (uk. 9), kuziharijia (uk. 12), n.k. Ametumia lugha yenye mafumbo kama vile: katika (uk.11) kuuelekezea ukuta konde, ukiona kwako kwaungua...(uk. 17).

Mhusika mwanamke pia ametumia msamiati ingawa sio kwa wingi. Alitumia: nimekinai (uk. 16) kudinda, ametumia msemo kama vile: kulia ngoa (uk. 16) katika kumaanisha kuwa alimwonea mama wivu ambaye mumewe hakai nyumbani kila wakati pia tangu jua kucha hadi lichwe (uk. 16) kumaanisha mchana mzima.

Wakati Mama na Mwanamke wanapozungumza, wanatumia lugha pevu inayokubaliana na umri wao na swala walilokuwa wakilijadili. Katika (uk. 16) Mama alipokuwa akimrejelea mumewe kama ngulusumu. Pia ametumia msemo kulia ngoa (uk. 16), methali ukiona kwako kwaungua..., msamiati kama vile stftahi, cha mchana na chajio, dengelua, fumbo kama vile: mdudu aliyejitosa sikioni hufahamika na mwenyewe anayehusika kumaanisha kuwa shida alizonazo mtu hazieleweki na mwingine na kila mtu ana shida zake. Msemo kupasuliwa mizungu (uk. 18) yaani wakamjulisha jinsi ya kulifanya jambo fulani hapa ikiwa ni kule kumpa mumewe dawa ya kumfanya atulie nyumbani asiwe kiguu na njia asiyejiali familia yake.

Wakati Mwanamke alipokuwa akijidai alivyoweza kumfanya mumewe atulie nyumbani, alisema:

Mwanamke: ... mbona nilipoibuka nilimzika janja
na hila zake na kumwopoa Zumbukuku
ulimwengu uko huku. (uk. 18).

Na aliendelea kusema:

Mwanamke: Sikutaka kubaki kitumwa
cha kumhangangaikia
mwanamume atakayebakia
gume gume la kumega
matonge tu. (uk. 16)

Lugha hii ina mnato kwa msikilizaji na inakubaliana na mazingira na hali wanayoizungumzia juu ya wanaume wasiozijali familia zao. Mama aliendelea:

Mama: ... hauvui mji kadamnasi. kuna mengi lazima
umezee Japo unabakia kuungulika ndani
kwa ndani ... zigo la simanzi lawatafuna
kama fuko (uk. 18)

Mtunzi wa tamthilia hii amefaulu katika kuwapa wahusika hawa lugha inayotarajiwa kwa watu wa umri huu na mada wanayoishughulikia. Wakati mama anapozungumza na watoto wake wadogo hatumii lugha yenyeye ukwasi huu wa mafumbo, methali, nahau n.k. bali anatumia lugha kavu kwa wingi na yenyeye msamiati rahisi unaoeleweka haraka na watoto wale hata ingawa wakati mwininge, lugha yake inakosa heshima na hekima.

Ingawa Mama wakati mwingine alitumia lugha ambayo haina heshima, alitumia mbinu ya tasifida anapoeleza yale yaliyomfika aliposhikwa na wale wapora ng'ombe na wakamnajisi.

Mama: ... mwenzangu (machozi yanaanza kumjaa)
nilitenzwa nguvu na... (uk. 22).

Mhusika Bosi pia tumemweka katika kundi hili la wahusika wazee wa makamo kwani ana umri wa miaka arobaini na saba. Huyu alitumia lugha tofauti na ile ya Mama na Mwanamke kwa vile yeye amesoma. Ni mhusika ambaye kama inavyotarajiwa, alitumia lugha ya mseto iliyoashiria hali yake ya kuwa amesoma na alifanya kazi katika afisi ya serikali.

Huyu ni mhusika ambaye ameathiriwa na lugha ya kigeni (Kiingereza) ambayo inatumiwa katika kufundishia na pia kama lugha rasmi. Alichanganya ndimi kwa kutumia Kiswahili na Kiingereza katika maongezi yake. Alitumia maneno kama vile: "leak", "reason", "to be afraid", "perfect", "disgrundled elements" n.k. (uk. 32).

Alitumia msemo wa Kiswahili maji ya moto hayachomi nguo. Alipokuwa akimaanisha kuwa, Jaribosi, ingawa alipinga mpango mbaya wa Bosi, hana uwezo zaidi ya kufanya makelele.

Bosi alitumia msamiati mwangi wa Kiingereza ulioonyesha kuwa alielewa msamiati wa kiuchumi katika uwanja wa kimataifa k.m "global village", "free market economy" na "individual enterprises". Ingawa hivyo yeye alitumia lugha ambayo haikubaliani na mamlaka yake. K.m alisema hivi:

Bosi: (Akichekacheka) Hii sio mali ya mamako! (uk 35).

Katika kuhitimisha twaona kuwa mtunzi wa thamtilia hii ya *Wingu La Kupita* amefaulu kwa kiasi kikubwa katika kuwapa wahusika lugha inayochukuana na kukubaliana na umri wao, elimu na kazi zao. Ingawa lugha hiyo inaoana na umri, kuna wale ambao wametumia lugha isiyo ya heshima hata ingawa wana umri wa kuheshimiwa.

LUGHA KATIKA MAZINGIRA NA MUKTADHA MAALUM

KATIKA WINGU LA KUPITA

Mazingira ni mahali, wakati na muktadha wa kijamii ambamo matukio ya kazi za kifasihi hutokea. Kanuni na uteuzi wa lugha huelekeza lugha iweze kujitofautisha katika mazingira na miktadha mbalimbali kwani lugha inayotumiwa katika mazingira ya harusi, mazishi , kanisa n.k huwa ya kipekee kulingana na mazingira hayo. Lugha ya mazingira fulani ikitumiwa katika mazingira mengine tafouti haitakuwa ya kufaa kwa mfano ikiwa mazingira ni ya furaha k.v harusi, tusitumie lugha ya huzuni na ikiwa ni mazingira ya huzuni tusitumie lugha ya kisherehe.

Katika tamthilia ya *Wingu La Kupita* kuna mazingira mbalimbali; tuna yale mazingira ya hali ya kukasirika k.m uhusiano baina ya mama na baba haukuwa mzuri kwa vile huyu bwana ambaye ni baba alikuwa amepuuza jukumu lake la kuishughulikia familia yake. Hakuwa akikaa nyumbani kama inavyotarajiwa kwa mume ambaye ana familia ya kutunza. Angekuwa akitulia nyumbani ili aweze kuelewa familia yake vizuri na pia aweze kuyajua matatizo ya kwake. Kinyume na matarajio haya, yeye hakai nyumbani. Amekuwa kiguu na njia. Jambo hili la kutotulia nyumbani na kutoijali familia yake linamfanya mama kumchukia mumewe hivi kwamba hataki kusikia mumewe akitajwa.

Jambo hili la kumchukia ndilo lililompelekea mama huyu kutumia lugha mbaya anapoambiwa na watoto wake kuwa mwalimu alikuwa amewaambia kuwa *baba ni mama* kwa maana kuwa mama na baba wanapaswa kushirikiana na kusaidiana na hivyo wanaweza wakamwuliza yejote kati yao (Baba na mama) swalii.

Mazungumzo kati ya mama na watoto yalikuwa haya:

Msichana: (Anajaliza usemi) Ehh mwalimu alisema kuwa
 baba na mama ni sawa. Nakumbuka sasa mama,
 mwalimu alisema baba ni mama. (uk. 1)

Mama: (Akionyesha kukanganywa na maneno ya msichana)

Ahh msiyafuate ya mwalimu wenu huyo, ana kichaa.

Tangu lini baba akawa mama. au kisomo cha siku hizi
ndivyo kilivyo? (kwa hadhira) kama si wazimu huo ni
nini basi? (uk. 1-2).

Maneno haya ya mama yanaashiria hali ya kuchukia na kukasirika. Maneno haya yanaoana vizuri na kuzorota kwa uhusiano baina ya mama na baba. Hatungetarajia mama huyu afurahie ile kauli ya mwalimu kuwa baba ni mama. Ingawa maneno haya yanaoana na hali hiyo mbaya baina ya mama na baba, hasira hizi za mama zinaelekezwa kwa asiyefaa, yaani mwalimu. Maneno makali haya yangeelekezwa kwa baba mwenyewe lakini tunachukulia kwamba mama anamwogopa baba kiasi cha kutoweza kumwambia maneno makali uso kwa uso. Na hivyo hasira zake zinaelekezwa kwa yejote anayesema mazuri juu ya baba.

Mwanzoni mwa tamthilia tunaelezwa kuwa mbegu zilikuwa zinatandazwa nje kukiwa na mawingu. Kwa hivyo ule wimbo wa watoto juu ya wingu na mazingira hayo ya kuweko na baridi kwa sababu ya wingu kufunika jua zinaoana vizuri. Watoto wanaimba:

Msichana na mvulana: Winguu ... winguu
Wingu ni jeusi wingu
winguu ... winguu
winguu kubwa zito
winguu. (uk. 3)

Kama tulivyosema hapo mbeleni kuwa uhusiano baina ya mama na baba haukuwa mzuri, tunapata mama akitumia lugha iliyoashiria mazingira au hali ya mtu anayejuta baada ya kufanya uamuzi ambao baadaye unamletea hasira na majuto. Hali hii tunaipata wakati wa mazungumzo baina ya

Mama na Mwanamke:

Mama: ... Kumbe kule kutaharaki kunioa ulikuwa ni kunilasia tu.
Kisha nami pumbavu ... Ndio nikamwamini haraka
lichya ya onyo la wajomba. (uk.9)

Maneno haya yanaoana vizuri na mazingira ya majuto na hivi ndivyo hali ilivyokuwa kwani mama huyu sasa anajuta na kujilaumu kwa kukubali haraka kuolewa na bwana huyu amabaye hatulii nyumbani wala kuijali familia yake kwa vyovyote. Wazazi walikuwa wamechoshwa na mikutano mingi waliyokuwa wakihudhuria shulenii. Hali hii iliwapalekea kudharau na kuchukia mikutano hiyo. Maneno yaliyosemwa na mhusika mama yanaoana na hali hii ya kuchukia na kudharau mikutano hiyo. Alisema:

Mama ... miye huko shuleni sikwenda, nimekinai mikutano
ya kila wakati. Siku zote hizo watoto wanasoma
hatusumbuliwi na mamikutano sasa ndio kunaratibiwa
nini siku hizi? (uk. 16).

Ili kuonyesha dharau na chuki dhidi ya mikutano hiyo ya mara kwa mara, mama alitumia Kiswahili kisicho sanifu ili kuonyesha hali hii. Aliirejelea ile mikutano kama "*mamikutano*."

Kama tulivyosema hapo mbeleni kwamba, watu waliosoma wameathiriwa na lugha ya Kiingereza sana katika mataifa yaliyoongozwa na wakoloni waingereza, tunaona kuwa kule kutoimudu lugha ya Kiingereza vizuri kunaashiria hali ya kutohitimu vizuri masomoni. Mhusika Mfungwa alitumia lugha ya Kiingereza vibaya. Alisema "MIF" badala ya "IMF" aliendela kusema "class strangle"

badala "class struggle" "Kerl Markise" badala ya "Karl Marx". "hit the head on the nail" badala ya "hit the nail on the head". Katika kumpa mhusika huyu lugha hii, mtunzi anatilia shaka kuhitimu kwake kimasomo. Mtunzi anataka kuonyesha kwamba kuna hatari katika kuwapa watu kama hawa nyadhifa wasizostahili. Kwani wanaweza kuperomosha uchumi wa nchi kwani hawaelewi madhara yanayoweza kuletwa katika jamii na vitendo vyao viouvu kama vile ufisadi ulioendelezwa na Bosi.

Mwishoni mwa tamthilia tunaona kuwa, baada ya mama kuambiwa mtoto wake amepigwa na askari wa chifu mle shulen i kwa kufuata mawazo ya mwalimu wao, mama alikasirika sana na akaona kuwa kitendo kile ni cha kinyama na hapo akatumia maneno haya:

Mama: sasa wanampigia nini mwana
 mkembe kama huyo?. (uk. 57).

Maneno hayo yanaoana na mazingira ya mtu aliyekasirika. Ingawa hivyo, twaona kuwa, Jaribosi ambaye alikuwa amesoma sana, alikuwa kifungoni kwa muda na asiweze kuwa pamoja na jamii yake. Aliporudi kutoka gerezani baada ya kumaliza kifungo, mamake (mama) anatumia maneno haya:

Mama: ... mwanangu nawe afya yako nayo
 imeishia gerezani. Heri umerudi hatimaye. (uk.57).

Katika hali halisi hatutarajii mama mtu ayatumie maneno kama haya baada ya mwanaye ampendaye kurudi kutoka kifungoni alikokuwa kwa muda mrefu.

Tungetarajia mama huyu atumie maneno ya kuonyesha furaha baada ya kuungana na mtoto huyo. Maneno haya ya mama kwa mwanawe Jaribosi kwa hivyo hayakubaliani vizuri na muktadha wa watu wawili wenye uhusiano wa karibu kama huu wanapoungana pamoja baada ya kutenganishwa kwa muda na kifungo cha jela.

Katika kuhitimisha sehemu hii ya matumizi ya lugha kulingana na muktadha, tunaona kuwa, mtunzi amefaulu kwa kiasi kikubwa katika kuitumia lugha vizuri kulingana na miktadha mbalimbali katika tamthilia ya *Wingu La Kupita*. Ingawa hivyo, tunaona kuwa, kuna sehemu, ingawa chache, ambapo alitumia lugha iliyopingana na muktadha. Kwa mfano lugha aliyoitumia mama baada ya Jaribosi kurudi nyumbani kutoka jela. Tungetarajia mama atumie lugha ya kuonyesha furaha kwa kuungana na mtoto wake ambaye walikuwa wametenganishwa na hali mbaya ya kifungo cha jela.

4.06 MATUMIZI YA LUGHA KITAMATHALI KATIKA WINGU LA KUPITA

Syambo na Mazrui (1992: xiv) wamefasili tamathali za lugha kama matumizi ya lugha ambapo maana hajitokezi au haiko wazi katika maneno yaliyotumiwa. Naye Mbatia, M. (2001:77) anasema kuwa, huu ni ukiushi wa kimakusudi wa matumizi ya lugha katika viwango vya maana (Semantiki) na mpangilio wa maneno (Sintaksia) ili kuleta maana mpya au msisitizo. Kwa hivyo tunaweza kusema kuwa, lugha huwa imetumiwa kitamathali wakati imetumiwa kwa namna ya kawaida kuashiria maana ambayo siyo ya kawaida. Kama Mbatia anavyosema, umuhimu wake huwa kusitiza au kuleta maana mpya.

Tamathali za semi za lugha huwa za aina nyingi. Kuna methali, misemo pamoja na miundo ya lugha aina mbalimbali ambayo si ya kawaida. Wakati dhana hizi zinapotumiwa vizuri katika mazingira yafaayo huwa zinatia ujumi katika lugha iliyotumiwa, huirembesha na kuiipa ufasaha na mvuto kwa msomaji. Kuna wahusika wa aina mbalimbali katika tamthilia ya *Wingu La Kupita*, kuna watoto, mama wa umri wa makamo na vijana kama vile Jaribosi ambao wamesoma. Kwa vile ina wahusika hawa tofauti ambao wamo katika mazingira tofauti, basi lazima wahusika hawa wawe na matumizi ya lugha yanayoonyesha tofauti zao za kiumri, kijinsia, kielimu na kikazi au tajriba.

Katika tamthilia, mtunzi ametumia misemo mingi ili kuendeleza mawazo yake kupitia kwa wahusika mbalimbali. Mwanzoni mwa tamthilia tuna mhusika Mama akizungumza na watoto wake nyumbani ambapo watoto wanataka kujua alipokwenda baba yao halisi. Katika maongezi haya mama aliwaauliza watoto hawa wakamwuliza baba yao wa kambo swali hilo lakini watoto walitumia msemo waliposema kuwa mwalimu aliwaambia kwamba, "*baba ni mama*". Maana aliyokuwa nayo mwalimu hapa ni kuwa wote wawili ni wazazi. Kutoelewa maana aliyokuwa nayo mwalimu, kulimpelekea mama kukasirika na kutumia msemo wa "mwalimu ana kichaa" (uk.2) kumaanisha kuwa mwalimu huyu ana kasoro ya kiakili.

Mama ametumia msemo kuwa, "watoto wake wana komango masikioni". Mama huyu alitumia maneno haya alipoambiwa na watoto wake kuwa baba yao wa sasa si baba halisi bali ni baba wa kambo. Jambo hili linamkasirisha mama kwa kuwa alikuwa amewaambia mara nyingi kuwa huyu baba ni sawa na baba wao wa awali na ndiposa akasema kuwa, "wana komanga masikioni" yaani hawaelewi. Anaendelea kutumia msemo kuwa "watoto wana vikokwa badala ya vichwa". Akimaanisha hawana akili na ndiposa hawashiki aliyokuwa akiwaambia.

Kuna wakati ambapo mama alikuwa akizungumza na mhusika Mwanamke alipotaka kujua ni nini yule mwanamke alichompa mume wake (mwanamke) ili atulie nyumbani. Mwanamke huyo alimwambia mama kuwa pengine kama angempa mumewe (baba) kile yule mwanamke alichompa wake, baba angeweza kumgeukia mama na "kuwa mbogo". Maana aliyokuwa nayo mwanamke huyo ni kuwa pengine baba atakuwa mkali zaidi kwa mama kuliko alivyo hivi sasa.

Mhusika mwanamke ametumia msemo huu: "kumvalia nguo" (uk. 18). Kwa maana ya kumchukulia hatua mumewe ili atulie nyumbani. Mwanamke huyu anaendelea na kutumia msemo kama vile "kumpasulia mizungu" (uk. 19) kwa maana ya kupewa siri au jinsi ya kukabiliana na hali

ile ya mumewe kutotulia nyumbani. Alipewa ujuzi huu na wanawake wengine waliokuwa wamewapumbaza waume wao.

Msemo mwingine uliyotumiwa na Mwanamke ni “moyo dimbwi lisilo kina”

(uk. 18) ambapo alikuwa akimaanisha kuwa hakuna mtu anayeweza kuelewa yaliyo moyoni mwa mwenzake, haswa matatizo anayoyapata kwani mwanamke huyu alidhania kuwa Mama hana matatizo ya kinyumbani lakini alipoelezwa na Mama jinsi anavyoteseka aliutumia msemo huo.

Katika kuonyesha sababu iliyomfanya marehemu babuye (mama) kuwalaki vizuri wageni walioingia kwao, mama alieleza kuwa, babuye aliongozwa na imani kwamba, “mgeni ni kama maji ya mto” (uk.19) maana aliyokuwa nayo mama ni kuwa, wageni huwa hawakai siku nyingi ugenini, wao hupita haraka kama maji yapitavyo.Hivyo, usiwakasirishe. Wageni wao hawakuondoka haraka lakini walikaa kwa muda mrefu mno. Wageni wao walikaa mpaka wakabadilika na kuwa wezi wa ng'ombe. Kitendo hiki kiliwahangaisha mama wasiweze kujua ng'ombe wao hupotelea wapi? Walienda mpaka kwa waganga lakini, hata waganga walishindwa kung'amua mwizi wa ng'ombe alikuwa ni nani. Ndiposa mama akatumia msemo kuwa “tunguli ziliwapiga chenga” yaani hata waganga walishindwa kutambua mwizi ni nani.

Mtunzi ametumia msemo “kupoteza matumaini” (uk.20). Msemo huu ulitumiwa na mwanamke pale ambapo mama alisema kuwa waganga walishindwa kung'amua mwizi ni nani. Katika kuieleza safari ndefu iliyofanywa na mama na jamii yake alipokuwa mtoto baada ya kutekwa mateka na wale wapora ng'ombe, mtunzi ametumia msemo wa “kitalifa kirevu” (uk. 22) kumaanisha safari ya umbali mrefu.

Baada ya kukauka kwa mti wa mgumo ambao ulikuwa kama madhabihu, mhusika mama, alitumia msemo, “ palisimikwa jengo” kumaanisha palijengwa jengo.

Anapoelezea ile hali ya waume wao kushindwa na majukumo yao ya kuzikimu jamaa zao sawa na alivyoshindwa Michonge, Mwanamke alisema kuwa, mumewe hatulii nyumbani hivi kwamba hata watoto wameanza “kumpiga vijembe” na kumsengenya wakati hayupo.

Kuna ule msemo wa “kujikaza kisabuni” (uk. 47) unaomaanisha kujitahidi au kuongeza bidii. Msemo huu ultumiwa na mama alipokuwa akiilaumu ile hali ya wanaume wengine kung’ang’ania uongozi hadi wazeeke kabisa.

Sio misemo tu ambayo imetumiwa katika tamthilia hii ya *Wingu La Kupita* bali tuna methali pia. Methali hizi zimetumiwa kupitisha mawazo fulani. Wakati mama anapoishutumu ile hali ya Jaribosi ya kushindana na mkubwa wake mpaka akafungwa jela. Yule mkubwa alitumia methali ya “*kuelekezea ukuta konde*” yaani kushindana na mwenye nguvu.

Wakati mwanamke anaponung'unukia ile hali ya mumewe kutoondoka nyumbani hata wakati mwanamke huyu anapofagia, mama anamjulisha mke huyu kuwa kuna wengine wenye matatizo mengi na makubwa zaidi ya hayo kwa kutumia methali:

“Ukiona kwako kwaungua, kwa mwenzio kwateketeta” (uk. 17). Kuna methali ya “Mungu si Athumanii” (uk. 28) kumaanisha kuwa Mungu si binadamu na hivyo yanayomshinda binadamu hayawezi kumshinda Mungu. Kuna methali ya “pwagu hupata pwaguzi” (uk. 30) inayomaanisha kuwa mwizi wa daraja la chini humpata mwizi wa daraja ya juu. Methali hii ilitumiwa na Jaribosi walipokuwa wakizungumza juu ya wizi uliofanyiwa umma na maofisa wakuu serikalini halafu tume ya uchunguzi ikateuliwa kuchunguza wizi huo lakini ile tume ikatumia takribani dola milioni ambazo ni mali ya umma pia. Hivyo wale wezi na ile tume sawa.

Jaribosi anapotaka kuleta wazo kuwa wakati wa kuondokewa na maovu utafika anatumia methali ya "liwike lisiwike kutakucha" (uk. 35). Katika tamthilia hii kuna mafumbo mengi yaliyotumiwa kwa mfano "mdudu aliyejitoso sikioni hufahamika na mwenyewe anayehusika" (uk. 18) kwa maana kuwa mtu ndiye anayefahamu uzito wa shida alizo nazo. Kuna fumbo la "nilipoibuka nilimzika janja na hila zake na kumwopoa zumbukuku ulimwengu uko huku" (uk. 18). Maneno haya yalitumiwa na mwanamke wakati alipokuwa akiirejelea ile hatua aligomchukulia mumewe ya kumfanya atulie nyumbani. Maana aliyokuwa nayo hapa ni kwamba ailimchukulia hatua na kumshinda.

Mwanamke yuyu huyu anasema hivi juu ya mumewe "gume gume la kumega matonge tu" (uk.18) kwa maana kuwa mumewe sio kama mwanamume bali mtu ovyo tu anayetegemea jasho la mwensiwe. Anaendelea kusema kuwa "jua hilo lilishawachwea wengine" (uk.18) kwa maana kuwa wengine walikuwa wameerevuka.

Kwa hivyo twaona kuwa mtunzi wa tamthilia ya *Wingu La Kupita* ameweza kutumia tamathali mbalimbali katika kupitisha mawazo yake. Lugha yake siyo kavu, ina mnato. Tunaona kuwa, wahusika wenye umri mkubwa wametumia tamathari nyingi kuliko wale wenye umri mdogo. Kwa mfano, mhusika Mama na Mwanamke ambao ndio wahusika wazee zaidi, wanaojitokeza hadharani katika tamthilia hii, wameweza kutumia lugha iliyo na tamathali nyingi na wengine kama vile Jaribosi wanaonyesha uwezo wa kuimundu lugha hata kutumia kinyume cha methali zilizozoleka katika kupitisha mawazo yao ili kuonyesha kuwa jamii ya sasa na ile ya zamani ni tofauti katika mitazamo yao ya maisha. Wahusika watoto wamepewa lugha kavu isiyo na msamiati mwingi na mafumbo. Ni kweli kuwa mtu hukomaa kilugha kama anavyokomaa kiumri.

4.07

MATUMIZI YA LUGHA KATIKA PANGO.

Tamthilia ya *Pango* ina wahusika wa aina mbalimbali. Kwa kuzingatia umri tuna wahusika watoto, vijana na wazee. Kwa hivyo tamthilia hii inaakisi wahusika halisi katika jamii halisi kwa vile kila jamii ina wahusika wa umri tofauti- watoto,vijana na wazee. Kuna jinsi watoto huitumia lugha, vijana wana yao na wazee huwa na yao pia. Tunaona kuwa katika hali halisi ya kijamii, watoto huwa na lugha nyepesi ambayo ina msamiati haba na sarufi rahisi. Huwa haina tamathali nyingi za usemi. Katika tamthilia ya *Pango* wahusika watoto ni Susa na Sota ambaao ni ndugu. Sota ana miaka kumi na moja na Susa ana miaka kumi. Kama inavyodhihirika katika tamthilia, watoto hawa wanatumia lugha nyepesi ambayo imekosa ukwasi wa msamiati mzito, mafumbo na tamathali nyingine za usemi, kwa mfano katika (uk. 5 – 6) wanapozungumza na Ngwese wanatumia lugha nyepesi. Katika (uk. 62-67) wanatumia lugha hiyo hiyo nyepesi. Ingawa hivyo, wametumia lugha yenye tamathali nyepesi hapa na pale. Katika (uk. 16) Sota anasema: “Ngwese alitufukuza kama ndege” Hapa ametumia tashbihi ambayo ni ya kawaida mno. Katika (uk. 33) ametumia tashbihi hii “nilifyatuka kama mshale” kwa maana ya kwenda kasi.

Tashbihi yake ya kwanza ni pale ambapo Ngwese aliwakataza kwenda kuteka maji kisimani na ile ya pili alitumia pale ambapo Katango na Kibwana walikuwa wakishambuliwa na mtu njiani. Kwa hivyo mtunzi amewapa watoto hawa lugha nyepesi ambayo inaafikiana na umri wao kwa vile wao hawajakua kilugha kwa vile umri wao ni mdogo. Mtu hukua kilugha kama anavyozidi kukua kiumri na kiakili.

4.08

LUGHA YA VIJANA.

Kama ilivyo kawaida katika hali halisi ya kijamii, vijana huwa wamekomaa kilugha kuliko watoto. Vijana haswa wa siku hizi, huwa wameibuni aina yao ya lugha inayowatofautisha na wazee. Jambo

hili mara nyingi huwa hivyo ili waweze kuhifadhi siri zao na pia waweze kujihisi kuwa wao ni vijana.

Katika tamthilia ya Pango, vijana wana lugha yao ya kipekee ambayo sio Kiswahili kwa mfano: katika (uk. 36, 39, 43 na 45) wametumia maneno haya: Wa! Wa! Wa! na aiwaal! aiwaal!. Maneno haya sio ya Kiswahili. Ni maneno ambayo wamebuni na wanayatumia wakati wa kushangilia. Pia katika (uk. 39 na 45) wametumia maneno po! po! po! ambayo ni ya kushangilia. Maneno haya hayatumiwi na wazee au watoto katika tamthilia nzima. Kwa hivyo ni maneno ya vijana hawa ambayo wameyabuni wenyewe. Yanawatofautisha wao na makundi yale mengine ya wahusika katika tamthilia.

Kama invyodhirika katika jamii yetu ya Kenya, vijana wana tabia ya kuitana kwa kutumia ufupisho wa majina yao. Kwa mfano katika (uk. 26), mhusika Katango anamwita Kikubi “*kub*”. Vijana ambao Wamitila amewatumia katika tamthilia yake ya *Pango* ni vijana ambao wamesoma. Kwa mfano Katango ni mwalimu na katika (uk. 25) Kikubi anasema walisoma naye Katango. Kwa kuwa wamesoma, elimu imewawezesha kuitumia lugha ya Kiingereza ambayo ndiyo lugha inayotumiwa mara nyingi katika kufundishia shulen. Hivyo wana ile tabia ya kuchanganya ndimi ili kurahisisha mawasiliano mionganoni mwao na pia waonekekane wao ni vijana waliosoma. Katika (uk. 24) Kikubi anatumia "*Mista*" badala ya neno la Kiingeereza "Mister". Hapa ametumia mbinu ya kutohoa maneno ya Kiingereza ili yachukue muundo wa maneno ya Kiswahili. Mhusika Mbabekazi ametumia neno “*Culture*” anasema kwa Kiingereza “we are not yet there!” (uk.25) Hapa ni alipokuwa akitaka kuonyesha jinsi itakavyokuwa vigumu kwake Katango kuweza kuchukua hatamu za uongozi. Ilhali mwanamke na jamii yao haidhamini mwanamke kuiongoza

Kwa vile wale anaowazungumzia hawaonyeshi kukanganywa na maneno ya kauli ile, basi tunajua kuwa hata wao wanaielewa lugha hiyo. Licha ya kutumia maneno halisi ya Kiingereza wameweza pia kuyatoho maneno mengine ya Kiingereza na hivyo kuyafanya yachukue umbo la maneno ya Kiswahili. Kama katika (uk. 25), Kikubi anasema "Stori" badala ya "story". Hapa alikuwa akimaanisha habari za kufurahisha zilizomo gazetini. Ametumia pia neno "*baibe*" badala ya "*baby*" maana aliyokuwa nayo hapa ni "msichana". Kwa vile vijana wana mazoea ya kuwarejelea wasichana kwa neno hili la "*baibe*".

Vijana hawa wamesoma na kuhitimu, haswa elimu ya sekondari. Tunasema hivi kwa sababu mhusika kwa mfano Katango ni mwalimu na hili linatufanya kuchukulia kuwa amesoma hadi sekondari na kujiunga na chuo cha mafunzo ya uwalimu. Kutokana na hali hii ya kuwa wamesoma, wamekomaa katika matumizi yao ya lugha. Lugha yao inaonyesha ukomavu huu kwa vile wanatumia lugha ilio na tamathali nyingi za usemi. Mhusika Katango ametumia fumbo anaposema kuwa, "ubinafsi Ukatutia kongwa" (uk. 9) yaani ubinafsi umewafanya viziwi wasiweze kusikia kilio cha wengine. Ametumia pia fumbo la "damu kuwa gundi ya ujamaa" kwa maana ya kuwaunganisha.

Alisema macho yake "sio madude ya kukamilisha urembo wa uso". (uk. 10) kwa maana kuwa, Ngwese asidhanie kuwa, Katango hakuwa ameyaona aliutowatendea ndugu zake. Ameonyesha ukiushi wa kisarufi anaposema "kulichoma letu pango" (uk. 15) badala ya kulichoma pango letu. Mhusika huyu pia ametumia methali ya "mbaazi uliokosa maua husingizia jua." Kwa maana kuwa, Ngwese anasingizia watu wengine anaposhindwa katika majukumu yake. Kuna matumizi ya misemo mionganoni mwa vijana hawa kama msemo "kulia ngoa" (uk. 13) yaani kuona wivu, "tabia ni kia cha mwili" kwa maana kuwa twapaswa kuwa na tabia nzuri.

Kikubi ametumia fumbo aliposema kuwa, “kondoo huvunja chungu ingawa hana pembe.” (uk. 28).

Kwa maana kuwa, usimdhara mnyonge kwa kutokuwa na nguvu kwani anaweza akasababisha hasara kubwa. Kikubi ametumia msemo kuwa “ndovu haangushwi kwa mshale mmoja” (uk. 28) kwa maana, wasikate tamaa katika kumwangusha Ngwese. Kauleni ametumia stiari ya “binadamu ni ngamba” (uk.53) yaani binadamu hatakosa kusema. Ametumia methali kuwa “Dua za kuku hazimpati mwewe.” Kwa maana, kelele za mnyonge hazimzuii mwenye nguvu kutenda mambo yake. Hapa ni pale alipokuwa akimhimiza Ngwese asiyajali maneno mabaya wanayoyasema watu juu yake (Ngwese).

Kwa hivyo tunaona kuwa vijana katika tamthilia hii ya *Pango* wameweza kuimudu lugha kwa viwango mbalimbali. Wanatumia lugha ya kipekee, ya mafumbo, misemo na methali. Pia wamechanganya ndimi. Hii inaashiria hali halisi haswa katika jamii yetu.

4.09

LUGHA YA WAZEE

Katika tamthilia hii Wamitila amewaumba wazee wa umri mbalimbali. Kuna wale wa umri wa miaka hamsini hivi na wengine walio na umri mkubwa wa zaidi ya miaka sabini. Katika jamii, wazee hutazamiwa kuwa na lugha ambayo ina utajiri mwingi wa mafumbo, methali, msamati, misemo n.k. Hii ni kutokana na sababu kuwa wana tajriba kubwa sana maishani na wamesikia wazee wengi waliowatangulia wakizungumza. Kwa hivyo tunatarajia wazee waweze kuitumia lugha ya kitamaduni yenyeye mapambo mengi ya lugha katika kupitisha ujumbe na mawazo yao.

Katika tamthilia ya *Pango* tunaona kuwa kuna baadhi ya wazee ambao wametumia lugha ya kishairi ili kusisitiza mawazo yao. Kwa mfano katika (uk. 8), mzee Ngwese anasema hivi: “Yangu Ndoto”badala ya “Ndoto yangu”. Anatumia misemo k.v “Miongo ya miaka” kwa maana ya miaka mingi (uk 14), stiari (uk 14) “*mimi ni kimbunga*” kwa maana, ana nguvu na uwezo na hivyo hatashindwa na mpinzani wake Katango katika kuchukuwa uongozi wa *Pango*.

Wakati mhusika Ngwese alipokuwa akiwafukuza Susa na Sota alisema kuwa "mali yangu sio ng'ombe wa kijiji kukamuliwa na kila mtu" (uk. 7). Hapa Ngwese ametumia stiari kwa maana kuwa hataki mali yake itumiwe na kila mtu humo kijijini. Anaendelea kusema, "ngoa inakutembea mwili mzima"(uk. 11) maana aliyokuwa nayo hapa ni kuwa Katango amejawa na wivu mwingu. Pia amesema "Umesikia wapi Katango maji ya mto kupanda mlima?" (uk. 11). Maana aliyokuwa nayo katika usemi huu ni kuwa ni jambo gumu sana kwake Katango kuweza kuchukua uongozi wa Pang'o sawa na ambavyo ni vigumu maji kupanda mlima.

Wakati mzee Ngwese alipotaka kuonyesha hajalishwi na maneno ya Katango alitumia msemo kuwa: "kelele za chura azimzuii ndovu kunywa maji" (uk. 12). Kwa maana kuwa asiye na nguvu hatamzuia mwenye nguvu kufanya lolote atakalo. Mhusika huyu ana utajiri wa kutumia aina mbalimbali za tamathali. Ametumia methali ya "kelele za mlango hazimnyimi mwenye nyumba usingizi." (uk. 13) . Maana aliyokuwa nayo ni kuwa, kelele na ushindani wa mpinzani wake Katango hautamzuia Ngwese kuendelea na shughuli zake za kushinda katika uongozi.

Mhusika mwingine aliye katika kundi hili la wazee ni Mama. Huyu ndiye mamake Katango, Susa na Sota. Ametumia methali kuwa "Ngoma ya wana haikeshi" (uk. 16) Maana aliyokuwa nayo hapa ni kuwa mambo yote ya vijana huisha haraka. Katika (uk. 16) ametumia fumbo alipokuwa akiwasuta Sota na Susa kwa kukaa sana kisimani. Anawauliza hivi "mligeuka Miche kuota huko mlikokuwa?" Anawafananisha na Miche kwa vile Miche hukaa ilipomea. Anawauliza pia kama kisima kimekuwa mchongoma (uk. 16). Mchongoma ni mti wenye miiba ambao kuupanda sio rahisi. Anatumia methali hii kwa maana kuwa wamechukua muda mwingi huko kisimani .

Seki ambaye ni babake Katango, Susa na Sota ni mionganini mwa wahusika wazee. Ametumia methali "Kichwa cha nyoka hakistahimili kilemba" (uk.20) maana aliyokuwa nayo ni kuwa Katango alitaka kuchukua jukumu kubwa la uongozi ambalo hawezi kulimudu. Ametumia fumbo kuwa "jicho litakalogueuka chongo huanza kutokwa na machozi mapema" (uk.22). Alitumia fumbo hili kumtahadharisha Katango kuwa kuna dalili ya mambo yatamharibikia Katango katika harakati zake za kuwania uongozi wa Pango. Mafumbo mengine aliyoyatumia ni kama vile: "upumbavu wa mjinga ndiyo busara yake" (uk . 19), " kiburi cha kuinua kichwa na kukigotesha jabalini kama mhusi" (uk.20). yaani maafa ya kujitafutia.

Mhusika Ngoro alitumia stiari nyingi kusifu nguvu za Ngwese. Anasema: "Ngwese ni kipunga", "ni shoka la kuikata miti mikinda" "ni mbogo" na "ni simba". (uk. 19, 21 na 23). Babu ndiye mhusika mwenye umri mkubwa zaidi katika tamthilia. Ametumia lugha ambayo ina mawaidha mengi kwa wale wadogo wake. Ina busara na hekima. Anatumia tamathali kuleta hali hizi zote. Katika (uk. 46) ametumia fumbo la "maua yamechanua na karibuni nyuki watarudi pangoni kuanza kutengeneza asali". Maana aliyokuwa nayo hapa ni kuwa kuna shughuli nyingi za kazi na hivyo wanapango wajiandae kwa kazi hizo. Anatumia msemo kuwa: "siku ya kujua mbichi na mbivu imefika, ya kutengeneza masega na nzana" (uk. 40). Anaendelea kutumia methali: "maisha ni matembezi kwenye daraja bovu" (uk. 57) yaani kuna hatari nyingi katika maisha na hivyo mtu ajihadhari nazo.

Baada ya Katango kushindwa na Ngwese, babu alimliwaza asikate tamaa. Alimwambia hivi: "mwewe anapochukua kuku wako, humrushii mayai". Alikuwa akimtahadharisha kuwa baada ya kushindwa asitende vitendo vingine vya kumletea hasara zaidi.

Mafumbo mengine ambayo ameyatumia ni, "uyoga wote huota mahali sawa lakini sio uyoga wote uliwao" (uk. 58) "na uchungu wa kujifungua hauwazui wanawake kushika mimba" yaani hata ingawa Katango ameshindwa sio kwamba hatawania uongozi huo mara nyingine.

Katika kuhitimisha tunaona kuwa mtunzi ametumia lugha yenyе utajiri wa msamiati na tamathali kaitka kupidisha ujumbe wake kupidia kwa lugha ambayo amewapa wahusika wake. Pia ameweza kuwapa wahusika wake lugha inayoambatana na umri wao, tajriba zao na elimu yao.

4.10 LUGHA KATIKA MAZINGIRA NA MUKTADHA MAALUM KATIKA TAMTHILIA YA PANGO.

Kuna mazingira na miktadha mbalimbali katika tamthilia hii. Kuna mazingira au miktadha ya furaha, siasa na ugomvi. Baada ya Ngwese kufunga njia kisimani kwa sing'enge Susa na Sota walijaribu kukifikia kisima hicho lakini Ngwese alishaona na akaanza ugomvi nao akiwakataza kupidia shambani mwake. Anatumia lugha yenyе dharau kwa watoto hao ili wajue amekasirika. K.m baada ya kuwauliza watoto hao walipokuwa wakienda, wao walimjibu kuwa walikuwa wakienda kisimani. Ngwese alirudia neno hilo kwa dharau. Alisema: "*kisi... mani?*" (uk. 5). Pia aliwafukuza kwa maneno haya:

Ngwese: (kwa hasira) ondokeni kabisa!

Hapa hamtakiwi kabisa

Nyie! (uk. 5).

Maneno haya yanaashiria na kudhihirisha mazingira ya hasira na ugomvi. Lugha nyingine ambayo pia inaashiria hali hii ni katika (uk 10-14) wakati Katango na Ngwese walikuwa wakigombana. Maneno yote katika sehemu hiyo yanaashiria mazingira ya ugomvi.

Baada ya Kauleni, Mbabekazi na Kikubi kukutana hotelini mwa Kauleni, walitumia lugha ambayo inaashiria hali ya furaha na ucheshi K.m Kikubi alimwuliza Kibwana aliye kuwa akisoma gazeti hivi:

Kikubi: (Akimwimanía) helooo!

Mister, gazeti linasema

ulimwengu utaishi lini? (uk. 24).

Lugha hii inaashiria mazingira ya ucheshi na utani. Katika maongezi baina ya Kibwana, Mbabekazi na Kikubi juu ya Katango. Lugha hiyo hiyo inayoashiria mazingira hayo ya furaha na ucheshi. Mazungumzo yao yalikuwa hivi:

Kibwana: Ni hii ya huyu mwenzetu

anayetaka kuliongoza Pango!

Mbabe kazi: Katango?

Kikubi: Ahh huyo? (mtuo) nimesoma

naye...Aliwahenyesha

wanaume ile mbaya

kutokana na misimamo yake.

Ana ujasiri sana beibe yule

Mbabekazi: Sema alikuhenyesha wewe...

Kikubi: Sio mimi aisee ni wengine. (uk 24-25).

Mazungumzo haya yanaoana vyema na mazingira yanapotumiwa yenye ucheshi pale hotelini.

Katika Uk. 37 – 49 lugha iliyotumiwa inaashiria mazingira ya kisiasa. Kwa mfano: wakati Ngoi alipomwuunga mkono Ngwese katika kampeni zake, anamsifu Ngwese.

Ngoi: Wa Ngwese yuko hapa wa
Ngwese kimbunga, yu hapa
wa Ngwese. Ngwese
shoka la kuikata miti
mikinda, wa Ngwese
mti uko tayari, wa
Ngwese shoka tia mpini
wa Ngwese kilele
kina pinda...(uk. 38).

Maneno haya yanazingatia vizuri muktadha wa siasa. Mtunzi ametumia lugha vizuri kulingana na muktadha na hali inapopatikana.

4.11 **MATUMIZI YA LUGHA KITAMATHALI**

Kama tulivyotangulia kusema katika sehemu ya matumizi ya lugha kitamathali katika thamtilia ya *Wingu La Kupita*, matumizi haya huondoa ukavu ama mfululizo wa ukawaida unaoweza kujitokeza katika lugha ya kawaida. Ndiyo ambayo huleta ufasihi katika kazi ya sanaa kama tamthilia. Lugha ambayo Wamitila ametumia katika kuendeleza kazi yake ni lugha iliyo na utajiri wa amali za tamathali na misemo. Amewapa wahusika wake lugha komavu inyooana na umri wao, tajriba na elimu. Amewapa lugha inayochukuana na mazingira mbalimbali; tunajua kuwa kulikuwa na ushindani wa kisiasa baina ya Katango na Ngwese. Pia kuna ushindani baina ya vijana na wazee. Vijana wakishikilia kuwa ni wakati wao na wana usasa kinyume na wazee ambao wanashikilia utamaduni yaani ukale.

Mzee Ngwese anataka kumdunisha Katango kwa kuwa Katango ni mwanamke kijana ambaye amesoma na kuwa mwalimu. Ngwese anatumia maneno haya:

Ngwese: Sitapoteza wakati wangu kutupiana maneno na mwanamke.

Ni hivi sikiliza, huo wivu wako... uukome! Najua umeurithi,
wazee wenu walimwonea babu wivu hivyo na hili halikumzuia
kuwa chifu: ni kelele za chura tu hazimnyimi ndovu kunywa maji:
ni kelele za mlango tu hazimnyimi mwenye nyumba usingizi.(uk. 13)

Lugha hii ina tamathali inayoaashiria hali ya dharau ya Ngwese kwake Katango.

Katango, katika kujitetea, alitumia methali alipomwambia Ngwese kuwa ameshindwa na uongozi lakini anazingatia mambo nje ya sababu za kushindwa kwake. Anatumia methali kuwa "Mbaazi uliokosa maua huzingizia juu".

Baada ya Katango na Kibwana kupigwa pale njiani walipokuwa wakitoka kwenye hoteli ya Kauleni mamake Katango alijaribu kumfanya Katango aachane na mchezo wa siasa ambao aliuona kama mchezo wa wajinga. Alimwambia Katango hivi: "wimbo wa mjinga huchezwa na wajinga wenzake" (uk. 34). Msemo huu ulikuwa wa kumwambia Katango kuwa yeze si mjinga kama Ngwese na hivyo aachane na siasa.

Wakati Kibwana alipokuwa akimhimiza Katango aendelee na siasa, alitumia fumbo kuwa, "yai viza huelea majini" (uk. 34). Alikuwa akimfananisha Ngwese ni yai lilo visa ambalo hutambuliwa na kila mtu kuona limeoza kwa kuelea majini. Ni kweli kwa sababu mwishoni mwa tamthilia, Ngwese alishikwa na polisi kwa kuwa alikuwa kufuja mali ya umma alipokuwa Mkurugenzi katika shirika la umma.

Kuna wahusika ambao wametumia lugha komavu yenyе mafumbo na misemo. Kwa mfano katika (uk. 12) Ngwese alimwambia Katango kuwa, “ ukelele wa shundi ni ule ule mmoja ” . Yaani Katango ni sawa na Jamaa zake ambao wamewaonea wivu akina Ngwese. Ngwese alimwambia Katango kuwa, "amemtegeea ndumba" (uk 13). Kwa maana kuwa Katango alitaka kumroga Ngwese ili afe na hivyo Katango aachiwe uongozi wa Pango. Kuna methali katika (uk. 13, 16, 34) na kadhalika tuna misemo katika (uk. 7,13,14, 28, 30, 32, 35) na kadhalika kuna mafumbo mengi katika tamthilia hii kwa mfano katika (uk. 1, 12, 16, 22, 48, 33, 57).Pia tuna stiari na tashbihi katika tamthilia hii ya *Pango*. Kwa hivyo tunaweza kusema kuwa lugha ya tamathali imetumiwa kwa wingi katika tamthilia hii na wahusika mbalimbali katika kuendeleza mawazo yao. Lugha hii inavutia na kunata makini ya msomaji na hivyo kuondoa uchovu ambao ungepatikana kama mtunzi hangetumia lugha kavu.

SURA YA TANO

5.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.01 HITIMISHO

Tasnifu hii imeshugulikia fani katika tamthilia mbili za K.W Wamitila: yaani *Wingu la Kupita* (1999) na *Pango* (2003). Vipengele ambavyo tumevishugulikia ni ploti, uumbaji wa wahusika na matumizi ya lugha. Katika tasnifu hii tumetoa mwishoni mwa kila sura maoni yetu kuhusu udhaifu ama ufanifu wa vipengele hivi, kama vinavyotokeza katika kazi hizi. Tumeitazama fani kama yenye kudhihirisha unafsia wa umbuji wa mtunzi kwa vile huwakilisha upekee wake wa utunzi. Kila fanani huwa na tabia ambazo anashikilia na kuzidhihirisha daima, na ambazo hawezi kuziachilia kwa urahisi.

Katika uhakiki wetu, tulidhamilia kujua kama uteuzi na matumizi ya vipengele mbalimbali vya fani alivyovitumia Wamitila, na jinsi alivyovitumia, vinaweza kuhusishwa na ufanifu ama udhaifu uliopo katika kazi zake. Tumeweza kubainisha kwamba nadharia hii ina ukweli. Ujumla wa upeo wa fani ambao tumejadili umetokana na uteuzi, matumizi, viungo na miundo mbalimbali ya kifani, athari zake za kisanii zikitathminiwa katika muktadha wa kanuni za utunzi wa tamthilia na zile za fasihi kwa jumla.

Nadharia tete yetu ya pili ilikuwa ni kwamba fani ya tamthilia ya pili yaani *Pango* ni pevu kushinda ya tamthilia ya kwanza (*Wingu La Kupita*). Kulingana na uchambuzi wetu tumeweza kudhihirisha kwamba ploti ya tamthilia ya pili *Pango* imeimarika zaidi kuliko ile ya tamthilia ya kwanza yaani *Wingu La Kupita* kwani ploti ya tamthilia ya pili ina

mgogoro wenyewe nguvu mbili kinizani yaani baina ya ushindani kati ya mhusika Ngweze na Katango ambapo tamthilia ya *Wingu La Kupita* haina mgogoro huu kama ambavyo tumeonyesha katika sehemu ya tathmini ya ploti katika tamthilia hiyo.

Tumeweza kubainisha kwamba nadharia tete yetu ya tatu haina ukweli tukizingatia tamthilia za Wamitila.

Kuna kule ambapo amevunja kaida za utunzi wa tamthilia kwa mfano kutumia kaida fulani sana (mtuo) na hivyo kushusha tamaa ya msomaji wa kazi hizi. Ingawa hivyo, kuna kule ameweza kufuata kaida fulani za utunzi wa tamthilia, kwa mfano kaida ya kitendo katika tamthilia ya *Pango*. Amebainisha lengo la mhusika Ngweze na Katango vizuri kutoka mwanzo hadi mwisho wa tamthilia hii.

Katika uhakiki wetu, tumekumbana na matatizo kadha. Tatizo kuu lililotukabili ni kuhusu malengo ya tasnifu yetu na uhusiano wake na mwongozo wa nadharia ya umuundo huagiza uchambuzi wa kazi ya fasihi kushughulikia vipengele na miundo ya fani iliyotumiwa bila kuihusisha na maswala ama sifa za nje za fasihi ama jamii. Kwa hivyo, mhakiki anayeifuata nadhalia hii katika uhakiki wake hana haja kurejetea maswala mengine kama vile maudhui.

Katika uhakiki wetu, hatungeweza kutenganisha fani na maudhui. Imetubidi tuhusishe uchambuzi wa baadhi ya maudhui kwa menajili ya kutathmini jinsi miondo ya fani imeweza kuchangia katika ukamilifu wa kazi za Wamitila. Sababu ya kutojitenga kabisa na maudhui katika mjengo wa kazi ya fasihi fani na maudhui ni kama mboni na jicho. Ni

vipengele ambavyo haviwezi vikatenganishwa. Katika kazi mbili za Wamitila kuna swala la ujisadi linalojitokeza. Swala hili linasababisha umaskini kwa jamii nzima na ndilo linalochangia katika kuanguka kwa wanaojihusisha nalo k.m Ngweze katika *Pango na Bosi* katika *Wingu la Kupita*. Swala jingine ambalo mtunzi huyo amelishughulikia ni lile la ubinafsi katika tamthilia zote mbili. Ameonyesha jinsi viongozi walivyojawa na ubinafsi na hivyo kutowajali watu wa tabaka la chini.

Ingawa amelishughulikia swala la nafasi ya mwanamke katika jamii, amewapatia nafasi tofauti katika tamthilia hizi mbili. Mhusika mkuu mwanamke katika tamthilia ya kwanza, *Wingu La Kupita*, amesawiriwa kama ambaye jukumu lake kuu ni kuzaa na kuwalea watoto lakini katika *Pango* mhusika mkuu mwanamke amejikomboa kimawazo na anajihuisha na maswala ya kisiasa ambapo anataka kuwa kiongozi wa nchi yake. Ingawa amewapa nyadhifa mbili tofauti amewaonyesha wakiwa washindi katika maisha.

Kuhusu kipengele cha uumbaji wa wahusika, Wamitila amewachora baadhi yao wakiwa hawana uhalsia wa maisha ya kawaida ya jamii. Kwa mfano, mhusika Baba haaminiki katika hali halisi ya maisha. Pia ushujaa wa wale watoto wawili katika *Pango* sio wa kuaminika.

Katika upande wa ploti inaonekana kwamba kuna baadhi ya matukio ambayo mtunzi ameyaingiza ambapo hayaeleweki viziri. Jinsi Wamitila amehitimisha tukio la mwisho la *Pango* na hata *Wingu La Kupita*, inadhihirisha udhaifu wa visa hivyo.

Katika tamthilia ya *Pango* mtunzi amekirahishisha kisa cha uchaguzi hasa wa kiongozi wa nchi sama. Hata jinsi Katango alikuja kuchukua hatamu za uongozi ni kitendo kisicho na uhalsia katika jamii za kisasa

Katika kukamilisha tungependa kupendekeza kwamba, wahakiki wengine wanaweza kuvishughulikia vipengele vingine kama vile mtindo na pia maudhui katika tamthilia hizi mbili za Wamitila na pia wengine waweza kushughulikia fani lakini kwa kufuata nadharia nyingine tofauti na tulioitumia.

MAREJELEO

Barry, P. (1995) Beginning Theory: An introduction to Literary and Cultural Theory. Manchester: Manchester University Press.

Culler, J.D. (1975) Structuralist Poetics. Oxford: Claredon Press.

Gill, R. (1985) Mastering English Literature. London: Macmillan Educational Ltd.

Kiteki, B.N. (1998) Uhakiki Wa Fani Katika Tamthilia Za E. Mbogo. Tasnifu ya M.A.Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Mbatia, M. (2001) Kamusi /Ya Fasihi: Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Msokile, M. (1993) Misingi Ya Uhakiki Wa Fasihi. Nairobi; English Press Ltd.

Mwangangi, M. (1996) Uhakiki Wa Fani Katika Tamthilia Za Jay Kitsao. Tamthilia Ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi.
(Hakijachapishwa)

Ngara, E. (1990) Ideology and Form In Africa Poetry. Nairobi: Heinemann Publishers.

Njogu, K; Chimerah, R. (1999) Ufundishaji Wa Fasihi: Nadharia Na Mbinu- Nairobi; Jomo Kenyatta Foundation.

Njuguna, N. (1996) Uhakiki Wa Fani Katika Riwaya Za Katama Mkangi. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi.
(Hakijachapishwa).

Packard, W. (1997) The Art Of The Playwright. New York:
Thunders Mouth Press.

Pemberstone Billings, R.N. (1965) Teaching Drama. London:
University of London Press.

Senkoro F. E. K. (1984) Fasihi: Dar-es-salaam: Press and Publicity Center.

————— (1997) Fasihi na Jamii. Dar-es-salaam: Press and Publicity Centre.

Syambo, B; Mazrui, A (1992) Uchambuzi Wa Fasihi. Nairobi: East Africa Educational Publishers.

Wamitila, K.W. (2000) Uhakiki Wa Fasihi Misingi na Vipengele Vyake. Nairobi: Phoenix Publishers.

————— (2003) Kamusi Ya Fasihi: Istilahi Na Nadharia. Nairobi: Focus Publications Ltd.

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

JOMO KENYATTA MEMORIAL
LIBRARY